

KITENGO CHA
MASHUJAA WA IMANI
SHULE YA JUMAPILI
KITABU CHA MWALIMU
Kwa umri wowote

# MASHUJAA WA IMANI

**Mtaala wa Shule ya Jumapili kutoka "Watoto ni Muhimu"**

**Kitabu cha Mwalimu**

**Kwa umri wowote**

**Kitengo cha 3: Masomo 1-13 (27-39)**

**Wavuti: www.WatotoAreImportant.com/heroes/**


## SHUKRANI KWA WOTE KATIKA TIMU YA "WATOTO NI MUHIMU"!

Mhariri: Kristina Krauss

Timu ya Ubunifu: Abril Palacios Camacho, Areli Zuriel Salinas Sanchez, Marlon José Hernández, Ramón Martínez García, Dwight Krauss, Flor Boldo, Jennifer Sánchez Nieto, Julio Sánchez Nieto, Mike Kangas, Suki Kangas, Verónica Toj, na Vickie Kangas.

Shukrani kwa Rubén Dario kwa muziki wa ajabu katika programu hii.

Timu ya Tafsiri: alineviera, Annupama Wankhede, Anton Klymyk, Araz Mammadzadeh, Aroma Publications and Media, Arturo Jr Boron, Blessy Jacob, Carmela Dawn Flores, Chrisbresnahan, David Raju, Ephraim Njuguna Mirobi, Finny Jacob, Geenav, HamidReza Azimi (hamid.azimi1364 at gm#ail com), Heyaudrey, I-clever.com, iqbalman, Jacob Kuruvilla, kamilturk, Karunguru Mwangi, kiran, Maitrayi Mondal, Marco Chu, Marcos Rocha, Mathew Das, Mitesh Mandaliya, mrramlama, Mrs.Geethashree NavaneethaKrishnan, Nassim Bougtaia, nicbenk, Paul Mwangi, Paul Septan, Rana922, Rubina Rai, Safdar Khan, shahroshan15, Talento-Unido, ueritom, Verdia Juliansyah Cancerika, Yeoh Jung Chin, Zeina Mirella Barzaga Arencibia

# UTANGULIZI

**KARIBU!** kwenye kitengo cha 3 cha shule ya Jumapili ya "Mashujaa wa Imani!"

"Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; tupige mbio kwa ustahimilivu katika mashindano yaliyowekwa mbele yetu." Waebrania 12:1

Mashuhuda waliotajwa katika fungu hili ni wale walio kwenye orodha ya 'mashujaa' wanaopatikana katika sura ya 11 ya Waebrania, mashujaa walewale ambao tumejifunza mwaka huu! Ni kama mashujaa hawa wote wanaweza kutuona hivi sasa, na ni zamu yetu kukimbia mbio. Sasa tuko hai hapa duniani, na tuna kitu cha kumpa Mungu. Majukwaa ya uangalizi yamejaa mashahidi wakitutazama tunapokimbia. Ni wakati wa kusonga mbele! Tuna miaka michache tu hapa duniani kuleta mabadiliko, na ni wakati wa kufanyisha kazi imani yetu!

Sio kila mtu atakuwa na fursa kama iliyokuwa na Musa ya kuzungumza moja kwa moja na rais wa nchi, akiwakilisha watu wa Mungu; wala hatutaweza kuokoa watu wa Mungu kupitia sherehe zenye chakula kingi na nguo nzuri kama alivyofanya Esta. Lakini kila moja ya hadithi hizi zina jambo muhimu ambalo tunaweza kujifunza katika maisha yetu ya leo. Ni muhimu tujifunze kuchukua hatua kama alivyofanya Mfalme Hezekia na Nehemia, na kama Ayubu tutii hekima ya Mungu ambayo ni zaidi ya yetu, kwamba tuzingatie uzima wa milele kuwa muhimu zaidi kuliko hata jinsi Shadraka, Meshaki na Abednego, walivyouchukulia na kwamba tusijaribu kukimbia mbali na Mungu kama Yona alivyofanya. Je, si tunapaswa kujifunza kutoka kwa mashahidi wengi hawa? Wacha tutumie imani yetu, na 'tupige mbio kwa ustahimilivu katika mashindano yaliyowekwa mbele yetu!'

Mungu abariki maisha yako kwa kuwaongoza watoto walio karibu nawe ili kushuhudia maisha ya "Mashujaa wa Imani."

Kwa Upendo,

Timu ya Watoto ni Muhimu







YEAH!!

# JINSI YA KUTUMIA NYENZO HII

## MSTARI WA WAKATI

Kila wiki watoto wanachora mstari kwenye mstari wa wakati katika vitabu vyao ili kuwakilisha maisha ya shujaa wa hadithi ya Biblia. Kwa mfano, katika somo la 1, wanapata maisha ya Elisha kwenye mstari ulio na namba 1 katika somo la 1. Kwa kutumia namba zinazotolewa katika somo, watoto wanapaswa kubaini mwanzo wa mstari na urefu wake. Kila mraba unawakilisha miaka 100. Kwa mfano, maisha ya Elisha yanaanza kati ya 800 hadi 900 K.K. na kuishia karibu 800 K.K. Itafurahisha kuona maisha ya kila shujaa na maelezo ya kushangaza, kama ukweli kwamba Shadraka, Meshaki na Abednego walitupwa katika tanuru wakati wa Yeremia.



# 1. CHUKUA HATUA



**Hadithi ya Bibilia: Elisha**
1 Wafalme 19:19-21, 2 Wafalme 2:1-18

## MSTARI WA KUMBUKUMBU 1

Luka 11:10 Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa.

## HADITHI YA 1 YA UHITAJI



Chumba cha shule cha Jumapili hakikupendeza sana. Hakikuwa kimepakwa rangi na baadhi ya kuta zilikuwa zimechakaa kidogo. Siku moja Kip alianza kutazama chumba kile na akahisi masikitiko, lakini akasema, "Nahitaji kuchukua hatua. Nitanunua rangi ili nipake chumba hiki." Kip alikuwa akihifadhi pesa kwa miezi mingi ili aweze kununua mchezo wa video, kwani anaipenda sana. Alipohesabu pesa alizokuwa amehifadhi, akaona kwamba ni kiasi sawa na kilichohitajika kwa ajili ya rangi na brashi. Je, angeweza kutoa pesa alizohifadhi kwa ajili ya mchezo wa video ili zitumike kanisani?

## SOMO KUU LA 1

Karibu tena katika Mashujaa wa Imani! Imekuwa ya kushangaza kuona jinsi Mungu aliovojidhihirisha katika maisha ya watu katika historia yote. Hebu tuangazie mifano mingine zaidi ya imani ambayo tunaweza kujifunza katika maisha yetu. Kumbuka hadithi kutoka wiki mbili zilizopita ya Eliya na mjane na kisha manabii wa Baali kwenye Mlima Karmeli? Leo tutajifunza kutoka kwa mrithi wake anayeitwa Elisha. Wakati Elia alipomchukua Elisha kama mtumishi wa kibinafsi, Elisha alitoa ng'ombe kama dhabihu na akachoma plau yake. Jibu lake kwa wito wake wa huduma lilikuwa kuchoma vifaa katika kazi na maisha yake ya zamani. Huo ndiyo ukali ambao Mungu anapenda. Yesu alituambia kwamba itatugharimu tunapoamua kumfuata. Je, tuko tayari kumweka mbele katika maisha yetu kabla ya kitu kingine chochote? (Luka 14: 25-35) Baada ya muda mfupi, ilikuwa wakati wa Eliya kuondoka duniani na kwenda mbinguni. Aliendelea kumshinikiza Elisha aende zake, na kumwambia akae mahali pengine wakati Eliya alisonga mbele. Elisha hakukubali. Alichukua hatua, akafanya zaidi kile alichoombwa , na akaendelea kusafiri pamoja na mtawala wake. Walipofika katika mto wa Yordani, Elia akapiga kwa kutumia vazi lake, na maji yakagawanyika ili wapite! Jambo hili limetendeka mara chache tu katika Bibilia. Walipokuwa wakitembea, Elia alimuuliza Elisha alikuwa akitaka nini. Elisha alionyesha kupiga hatua tena, akaomba kitu cha ujasiri: sehemu maradufu ya roho ya Eliya. Elia akajibu kwamba ikiwa angeendelea kuwa mstahimilivu na awepo wakati "anafariki," basi angeipata. Eliya alikufa kwa njia ya kushangaza sana. Badala ya kufa kama kawaida, gari la moto lilikuja chini na kumchukua na kwenda naye mbinguni! Elisha akachukua vazi la Eliya na kurudi. Katika mto wa Yordani, alichukua hatua na kupiga maji jinsi Eliya alivyofanya, na maji yakagawanyika tena! Alikuwa na imani kwamba Mungu angemjibu na kwamba angepewa kile alichoomba.

Tunashuhudia watu wanaochukua hatua katika Agano Jipya, pia. Petro alimwambia Yesu amwite ili atembee juu ya maji, naye akafanya hivyo! Mwanamke Mkanaani aliendelea kumwomba Yesu amponye binti yake. Yesu alipomwambia kwamba ametumwa kwa Waisraeli pekee, alimwomba tena, akisema ni

jambo ndogo sana na rahisi kufanya, na binti yake akapona.Mkuu wa jeshi alimwomba Yesu amponye mtumishi wake. Na akimtambua Yesu kama Mfalme na mamlaka ya juu katika ulimwengu, alimwombe Yesu asiende nyumbani mwake bali aseme tu neno, na mtumishi wake angepona. Hii ndio aina ya imani ambayo Mungu huzawadi. Yesu alituambia kwamba ikiwa tuna imani ndogo tu kama mbegu ya haradali, hakuna kitu kitakacho tushinda. (Mathayo 17:20)

Nitachukua hatua na kutumia imani yangu katika vitendo.

## SULUHISHO LA 1



Akaenda na kununua rangi na brashi. Siku moja wakati hakukuwapo na madarasa, alienda na akapaka rangi chumba. Mwalimu alipogundua, alimpongeza Kip kwa hatua ambayo alikuwa amechukua. Baada ya hatua hio waliunda timu kwa ajili ya matengenezo ya chumba na wakamchagua Kip kama kiongozi wao.

## SHUGHULI YA 1

**Kuchukua hatua**



Unda orodha ya mambo ambayo wanafunzi wanaweza kusaidia, kama vile kusaidia mwanafunzi mwenzao na kazi ya ziada au kusafisha nyenzo baada ya shughuli ya darasa. Unaposhuhudia watoto 2 au 3 wakifanya hivyo, wapongeze. Alika kila mtu awape pongezi kwa kuwapigia makofi. Sema kuwa msaada wao unaashiria hatua yao ya kutenda mambo. Waombe wafikirie kuhusu mambo wanayoona nyumbani au shuleni mwao na waandike jambo moja ambalo wanaweza kusaidia na uwaombe walieleze katika wiki inayofuata.


## MSTARI WA 1 WA WAKATI


Kwa kutumia maelezo kutoka kwa maswali, ongeza Elisha kwenye mstari wa wakati.

Je, Elisha alichukua nafasi ya Eliya katika mwaka gani? Jibu: Karibu mwaka wa 850 K.K.

Je, Elisha alikufa katika mwaka gani? Jibu: Karibu mwaka wa 788 K.K.

## MAJIBU 1 YA MAFUMBO








## MASWALI NA MAJIBU YA 1


**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, unahitaji kusubiri mwito wa Mungu KABLA kabla ya kuanza kufanya kazi nzuri? Ikiwa sivyo, kwa nini?
   Wacha wanafunzi wajadili jambo hilo. Je, unaweza kuwa mmishonari bila kupokea mwito maalum? Je, tunaweza kumpa mtu maskini glasi moja ya maji bila Mungu kutuomba? Je, tunapaswa kuchukua hatua kwa kiasi gani katika mambo ya Mungu? Je, unaweza kuuza gari lako na kutoa kila kitu kwa ajili ya huduma? Je, unaweza kuuza nyumba yako na usafiri hadi nchi nyingine ili kuhudumu bila mwito maalum?
2. Je, utiifu kwa Neno la Mungu kwenye Bibilia unasababisha nini? Na ni lini ni muhimu kupokea mwito kutoka kwa Mungu mbali na yale ambayo tayari yameandikwa katika Maandiko?
   Kwa upande mmoja, tunapaswa kutenda kila wakati kulingana na yale tunayojifunza kutoka kwa Bibilia ambayo Mungu anatuomba tufanye. Kuna msemo unaosema kwamba rahisi kubadili mwelekeo wa gari wakati linasonga kuliko wakati limeegeshwa. Ni bora kuanza KUFANYA JAMBO KWA AJILI YA MUNGU, na kutoka hapo Mungu anaweza kutuongoza. Kwa upande mwingine, tunapokua Wakristo waliokomaa, ni vyema kumtii Mungu kwa chochote mahususi anachotuomba tufanye au tusifanye. Jambo linaweza kuonekana kama wazo nzuri, lakini Mungu anaweza kuwa anataka mtu mwingine alishughulikie na anaweza kuwa na jambo lingine kwa ajili yako. Unapoendelea kukua, jifunze kutambua ikiwa unapaswa kupiga hatua mbele peke yako au unapasa kusubiri maagizo ya Mungu.
3. Je, Mungu anapenda hatua ya aina gani?
   Ulimwenguni kote, makampuni makubwa yanapendelea wasimamizi wanaochukua hatua. Inamaanisha kwamba wanawajibikia nafasi zao na huwa hawasubiri mtu kuwaeleza cha kufanya. Wao hubuni hatua wanazohitaji kuchukua ili kuboresha bidhaa zao. Wafanyikazi ambao wanasubiri tu kuelezwa cha kufanya na kamwe hawafanyi mambo ya ziada au hawachukui hatua watasalia katika kiwango cha chini sana na hawafikia kiwango cha usimamizi. Je, hali hii inaweza kuwa katika huduma ya Mungu? Je, inawezekana kwa Mungu kutafuta 'wafanyikazi' kama kampuni ya Pepsi inavyofanya, kwa viwango tofauti kulingana na majukumu ya kila mtu?

## MCHEZO WA 1


**Mlipuko wa puto**

Ili kuandaa, ingiza vipande vidogo vya karatasi ndani ya puto na kisha uweke pumzi. Tumia karatasi za rangi 3 ili karatasi nyeupe iwe na thamani ya alama 2, kijani kibichi iwe na thamani ya alama 4, na bluu iwe na alama 6. Unaweza kubadilisha rangi hizo kama inahitajika. Ili kucheza, gawanya darasa kwa timu. Kwenye ishara yako, watoto wanazunguka huku wakilipua puto na kukusanya karatasi ndogo ndani yake. Timu itakayokuwa na alama nyingi inashinda. Zingatia kutoa zawadi ndogo wa timu inayoshinda.



## MAHUDHURIO YA 1

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:




**Elisha**

## KAZI YA 1 YA NYUMBANI

Chagua mtu mzima wiki hii ambayo unaweza kujifunza kutoka kwake na ujitoe ili kumsaidia bila yeye kukuomba. Inaweza kuwa mchungaji, mwalimu, mzazi, au mtu anayekuvutia ambaye anaweza kukufunza kumfuata Mungu. Usiwaeleze wenzako kile utakachofanya, lakini uchukue hatua na ukifanye.

**Soma**

Siku ya 1: 2 Wafalme 4:8-13
Siku ya 2: 2 Wafalme 4:14-19
Siku ya 3: 2 Wafalme 4:20-26
Siku ya 4: 2 Wafalme 4:27-31
Siku ya 5: 2 Wafalme 4:32-37

# 2. POKEA BARAKA



**Hadithi ya Biblia: Mwanamke wa Shunemu**
2 Wafalme 4:8-37, 8:1-6

## FUNGU LA 2 LA KUMBUKUMBU

Waefeso 3:20 Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;

## HADITHI YA 2 YA UHITAJI



Peppy amekuwa akiomba ili apate vifaa vya maabara. Siku moja aliona kuwa jirani yake, mwanamume mkongwe, alikuwa akisafisha bustani nje ya nyumba yake. Kulikuwa na magugu mengi kwenye bustani hio, na Peppy aliona itakuwa kazi nyingi kwa jirani yake kuisafisha akiwa peke yake; kwa hivyo akauliza ikiwa angeweza kusaidia na mtu yule akakubali.Walitumia siku karibu nzima wakisafisha bustani na walipomaliza, mtu huyo aliomba kujua nini Peppy anapenda zaidi. Peppy alimwambia kwamba anapenda kufanya majaribio ya kisayansi.

## SOMO KUU LA 2

Karibu tena katika Mashujaa wa Imani! Leo tutaangazia mtu ambaye alionyesha ukarimu kwa Elisha, mtu wa Mungu. Mwanamke wa Shunemu pamoja na mumewe walimkaribisha Elisha nyumbani kwao kila wakati alipopita karibu na eneo hilo na hata waliunda chumba kwa ajili yake. Iliwagharimu muda, pesa na juhudi ili kuonyesha ukarimu kama huo kwa Elisha. Yesu aliweka wazi kuwa anapenda watu wake na mambo tunayowatendea watu wake, anayachukulia kana kwamba tumemtendea Yeye (Mathayo 10: 40-42). Lakini hatuwezi kamwe kumbariki Mungu! Mambo yote ma mazuri unavyowafanyia wengine, Mungu atakufanyia vitu vikubwa hata zaidi, mengine hapa duniani na mengine mbinguni. Walijenga chumba kwa ajili ya Elisha, hatua ambayo ni zaidi ya kile mtu wa kawaida anaweza kufanya, lakini lilikuwa jambo ndogo sana ukilinganisha na njia nyingi ambazo Mungu alibariki mwanamke wa Shunemu! Elisha alishukuru sana kiasi kwamba alitabiri mwanamke huyo atapata mtoto wa kiume. Alisita kuamini na kupokea baraka kuwa jambo kama hili lingetendeka. Mungu anapotubariki, wakati mwingine inaonekana kubwa sana na ngumu kuamini! Lakini wakati Mungu anapochagua kukubariki, mwamini Mungu tu na ukubali. Mruhusu Mungu akuonyeshe jinsi anavyokupenda; na anakupenda sana.

Miaka kadhaa baadaye, mtoto alifariki siku moja. Angeanza kuhuzunika papo hapo. Angemkasirisha Mungu kwa maumivu yote katika wakati huo. Angeweza kumlilia mumewe. Badala yake, alikwenda moja kwa moja kwa Elisha, na kuomba usaidizi wa Mungu. Elisha alikwenda pamoja naye na akamwomba Mungu, na mtoto akafufuka! Je, unamwamini Mungu kuwa anaweza kutunza baraka ambazo amekupa? Wakati mambo mabaya yanatokea, je, utamwomba Mungu akusaidie? Yeye anakupenda sana! Yeye anataka kukutunza na kukubariki katika nyakati nzuri na mbaya. Kama mwanamke wa Shunemu, nenda kwa Mungu kwanza na uombe usaidizi.

Elisha akamwonya mwanamke wa Shunemu aondoke nchini kwa miaka 7 kwa sababu ya ukame. Waliporudi na kwenda kwa mfalme kuomba ardhi irejeshwe, kitu cha kushangaza kilitokea. Walipokuwa

wanaingia, mtumishi wa Elisha alikuwa akimweleza mfalme hadithi kuhusu Elisha, pamoja na jinsi aivyoweza kufufua mvulana wa Shunemu.Mungu hata alitumia jambo mbaya lililotokea ili kuendelea kumbariki katika maisha yake yote. Ikiwa mvulana hengekufa na kufufuka, hakuna hadithi yoyote ya kushangaza ingeelezwa. Mfalme alimuuliza kuhusu kisa hicho na alihakikisha familia yake haikurejeshewa ardhi tu lakini pia pesa kutokana miaka 7 ya mavuno kutoka kwa ardhi hio! Unaweza kuamini upendo wa Mungu juu ya maisha yako na kukubali baraka zake kwako.

Ninachagua kuwatendea mema wengine na ninakubali upendo na baraka za Mungu kwangu.

## SULUHISHO LA 2



Siku iliyofuata, jirani ya Peppy alifika nyumbani kwao akiwa na sanduku na kusema, "Hili ni lako.Fungua."  Wakati Peppy alifungua sanduku aliona kuwa ni vifaa vipya vya maabara.Halafu akasema, "Hapana, siwezi kupokea hili!"Jirani akasema, "Bwana aliniambia nikupe hili kama thawabu kwa kile ulichonifanyia." Peppy akajibu, "Lakini hii ni gharama nyingi sana!" Yule mtu akajibu, "Ni yako, nakupa."

## SHUGHULI YA 2

**Mikono ya ukarimu**




Chora mikono yako miwili kwenye karatasi. Hakikisha inaingiliana. Kata sehemu ya nje ya mchoro wa mikono na uikunje kama kijitabu kidogo. Nje ya kijitabu, mtoto anaandika jina lake. Katika upande wa ndani, andika mawazo kuhusu jinsi ya kuwa mkarimu kama mwanamke wa Shunemu kwa Elisha.


## MSTARI WA 2 WA WAKATI

Je, mwanamke wa Shunemu na Elisha walikutana mwaka gani? Jibu: Karibu mwaka wa 847 K.K.

## MAJIBU YA 2 YA MAFUMBO

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | G | N | U | M | A | E | K | O | P | O |
| F | K | M | S | O | O | A | M | V | I | B |
| A | M | A | J | O | N | Z | I | A | L | D |
| A | A | O | R | L | S | I | D | F | K | O |
| K | V | T | M | I | N | J | S | U | K | U |
| A | U | O | O | I | M | U | V | K | A | P |
| R | N | T | A | U | A | U | L | I | B | E |
| A | O | M | R | H | I | M | P | L | M | N |
| B | U | V | G | U | S | L | U | A | U | D |
| T | E | L | I | S | H | A | L | E | H | O |
| H | O | A | D | A | A | S | M | I | C | Y |






## MASWALI NA MAJIBU YA 2

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, ni mambo au hali gani ambazo zinaweza kuwa baraka zisizotazamiwa?
   Huenda hatuko tayari kupokea baraka kutoka kwa Mungu, mara nyingi kwa sababu hatutambui kuwa jambo fulani ni baraka. Kwa mfano, ikiwa wazazi wetu wataamua kuhamia mji mwingine, maisha yanakuwa magumu kwa muda katika eneo jipya. Lakini inawezekana mtakutana na mpenzi wako wa maisha katika mji huo mpya?
2. Je, ji gani ambayo Mungu anathamini zaidi, maisha yetu ya kiroho au ya kimwili? Ni aina gani ya baraka ambazo Mungu hutoa zaidi, ya kiroho au ya kimwili?
   Kwa mwanamke wa Shunemu, Mungu alitoa mfano wa baraka za kimwili. Lakini maisha yetu ya kiroho ni muhimu zaidi kuliko maisha yetu ya kimwili. Baraka bora zitakuwa kwa nafsi yako, sio lazima ziwe mali. Kwa mfano, kiburi kingi mno kitaathiri vibaya kazi zetu katika siku zijazo.
3. Je, ni baraka ikiwa Mungu anatupisha hali inayotufanya tuwe wanyenyekevu? NDIYO!!!

## MCHEZO WA 2

**Mpira wa voliboli kwa kutumia puto**



Watoto wote wanaketi kwa mduara na wametekanya miguu yao. Waambie watoto kwamba sasa wamegundishwa kwenye ardhini na wanaweza kusongesha kiwiliwili na mikono yao pekee. Tupa puto iliyojazwa pumzi katikati ya mduara. Watoto wanapaswa kupitisha puto kutoka kwa mtoto mmoja hadi mwingine kwa kupiga jinsi mpira wa voliboli unavyopigwa kwa kichwa. Ikiwa mshiriki ataangusha puto, anapoteza usongezaji wa mkono mmoja, kisha huyo mwingine, kisha kiwiliwili chao, kisha kichwa chao mpaka wamegandishwa kabisa na wanaondoka mchezoni.

## MAHUDHURIO YA 2




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Manabii Wandogo**

## KAZI YA 2 YA NYUMBANI

Tafuta namna kufanya kitu kizuri kwa mtu wiki hii, kama vile kusaidia mama yako kuwaakulia chakula wageni au kutoa vichezeo nyako kwa mtu mwingine. Pia, kuwa makini katika wiki hii ikiwa Mungu atakufanyia jambo nzuri. Ikiwa mtu anakufanyia jambo nzuri wiki hii, mshukuru ipasavyo na kisha umshukuru Mungu kwa faragha pia, kwa sababu Yeye ndiye chanzo cha vitu vyote vizuri katika maisha yetu.

**Soma**

Siku ya 1: 2 Wafalme 5:1-6
Siku ya 2: 2 Wafalme 5:7-10
Siku ya 3: 2 Wafalme 5:11-14
Siku ya 4: 2 Wafalme 5:15-20
Siku ya 5: 2 Wafalme 5:21-27

# 3. KUTII BILA KUELEWA



**Hadithi ya Biblia: Naamani**
2 Wafalme 5

## FUNGU LA 3 LA KUMBUKUMBU

Mithali 3:5 Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe;



## HADITHI YA 3 YA UHITAJI

Buzz alikuwa amealikwa kwenye maonyesho la vikaragosi, ilitajia kupendezwa sana! Marafiki zake wote walikuwa wakuwepo. Siku ya uwasilishaji, walitangaza kwenye runinga kwamba watacheza sinema kadhaa ikiwa ni pamoja na *Bambi* , ambayo ni kipendwa cha Buzz.Kisha akawaza, "Siwezi kukosa sinema, hata ingawa maonyesho ya vikaragosi hupependeza." Ilipofika wakati wa kwenda kwa uwasilishaji, marafiki wa Buzz walifika ili kumchukua.

## SOMO KUU LA 3

Karibu tena kaktika Mashujaa! Tutaangazia mtu maarufu leo ambaye alijifunza unyenyekevu na kumruhusu Mungu kuamua jinsi mambo yanavyopaswa kufanywa. Naamani alikuwa mkuu wa jeshi katika Aramu na aliheshimiwa na kila mtu. Alikuwa maarufu na mkuu. Ni rahisi unapokuwa maarufu na mkuu kutarajia Mungu akutendee kama mtu maarufu, lakini Mungu hana upendeleo. Naamani alichukua hatua sahihi kwa Mungu, kuacha matarajio yake yote ili kumfuata Yeye. Naamani alikuwa na ukoma, ugonjwa mbaya wa ngozi. Mjakazi wa mke wake aliwashauri waende Israeli mahali palipo na nabii wa Mungu. Naamani angeweza kupuuza msichana huyo mchanga, lakini badala yake aliamua kusikiliza na kufuata ushauri wake. Mungu anazungumza kupitia kila aina ya watu, na ikiwa hatutaki kusikiliza watu ambao kwa kawaida wanaonekana wandogo na wanyonge (ingawa mbele ya macho ya Mungu, sote tunafanana) basi tunaweza kukosa baraka za Mungu juu ya maisha yetu. Naamani alifuata ushauri wake na akaenda Israeli ili kutafuta usaidizi wa Mungu. Tena, nyumbani kwa nabii, Naamani alitarajia kutendewa kama mtu mkuu. Badala yake, nabii Elisha alimtuma mmtumishi wake amwambi aoge mara 7 katika mto Yordani. Naamani alikasirika, lakini aliamua kuwasikiliza watumishi wake wakati walimhimiza atii maagizo ya nabii. Usiruhusu kiburi chako kiwe pingamizi katika njia ya kumfuata Mungu, hata wakati hauelewi. Katika kitabu cha Mithali tunafundishwa kumtegemea Mungu badala ya kuamini uelewa wetu wenyewe (Mithali 3:5). Mto Yordani ulikuwa mchafu sana. Fikiria Naamani kama amesimama pale ndani ya maji. Karibu na kingo kulikuwa na ngamia zake zilizokuwa zimebeba dhahabu na utajiri na watumishi wake wote walikuwa wakimwangalia. Labda alijaribiwa kuacha kuoga baada ya mara 5 au 6, akifikiria ni upumbavu kufanya hivyo. Lakini badala yake, aliendelea kutii maagizo ya nabii na kuingia ndani ya maji mara 7. Kisha akapona! Alifurahi sana kwa kuwa mambo yote ambayo yalionekana kama ya kipumbavu hayakumtia wasiwasi tena. Unapoona muujiza ambao Mungu anafanya kupitia utiifu wako, mambo yote ambayo yalionekana ya kipumbavu hayatakujalisha tena. Naamani alirudi kumshukuru Elisha na kumpa zawadi zote ambazo alikuwa ameandaa. Lakini Elisha alichagua

kutenda kwa unyenyekevu pia na akakataa zawadi zote. Mtumishi wa Elisha aliyejulikana kama Gehasi hakuchagua unyenyekevu lakini alitamani hazina hio. Badala ya kuishi kwa furaha akiwa na hazina ya ziada, Gehasi aliishi na ukoma kwa maisha yake yote kwa sababu ya kitendo chake. Yesu alisema tuwe wanyenyekevu na tumruhusu Mungu atuinue badala ya kujiinua (Luka 14:11) Naamani alikuwa maarufu kwa muda mfupi kwa yote aliyoyatimiza katika jeshi la Aramu, lakini kwa maelfu ya miaka amekuwa maarufu ulimwenguni kote kwa utiiF wake kwa Mungu.

Ninachagua kusikiliza na kutii hata wakati sioni maana.

## SULUHISHO LA 3

Buzz aliwaambia kwamba hawezi kwenda kwa sababu sinema zilikuwa za kuvutia zaidi. Baada ya marafiki wake kusisitiza, alikubali kwenda. Katika tukio hilo, Buzz na marafiki zake walimpokea Yesu mioyoni mwao na maisha yao yakabadilika! Sasa alikuwa na furaha kutokana kile kilichokuwa kimetendeka.



## SHUGHULI YA 3

**Fanya kile ninachosema, sio kile ninachofanya**

Wanafunzi wote wanasimama kama kikundi na mwalimu anasimama mbele yao. Mwalimu anaanza kutoa maagizo ya mdomo ili kugusa sehemu ya miili yao, kama vile pua, goti, nywele, nk. wakati anagusa sehemu tofauti ya mwili wake. Kwa mfano, mwalimu anasema waguse vichwa vyao ilhali anagusa goti lake. Watoto ambao wanafanya makosa wanatoka nje ya mchezo na kuketi.




## MSTARI WA 3 WA WAKATI

Je, Naamani aliponywa ukoma katika mwaka gani? Jibu: Karibu mwaka wa 830 K.K.

## MAJIBU YA 3 YA MAFUMBO








## MASWALI NA MAJIBU 3

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

2. Je, kwa kweli Mungu atatuzawadi kwa kazi zetu hapa duniani?
   Wakati mwingine kwa kukosa imani, tunakuwa wavivu kutekeleza ahadi za Mungu. Tunaona kuwa dunia haina haki na kudhani hata mbinguni itakuwa bila haki na tunapoteza motisha kwa kazi yetu hapa duniani. Ongea kuhusu dhawabu tofauti na yale ambayo wanafunzi wanaweza kufanya ili kupata dhawabu hizo.
3. Je, ni mambo gani unaweza kufanya ili upate simu mpya?
   Ili kusisimua zaidi, jadili ni mambo gani ambayo ungefanya. Wacha wafikirie kuwa labda Mungu atatupa dhawabu hizo za kiteknolojia. Mungu alisema kuwa mbingu na thawabu zitakuwa bora kuliko tunavyodhania... kwa hivyo Mungu anaweza kutushangaza na thawabu za kiteknolojia! Kwa mfano, huko Guatemala waliunda mashindano ya kushinda iPad ya hivi majuzi. Washiriki walilazimika kufanya jambo kubwa zaidi ili kustahiki tuzo hilo. Msichana alikula nyungunyungu alye hai na akashinda! Yuuuck. Je, unaweza kumfanyia Mungu nini?
4. Je, Mungu angekuomba ufanye jambo ambalo hutaki kufanya, unaweza kulifanya! Je, utapata dhawabu yake?
   Kumbuka jinsi Naamani alivyokasirika wakati nabii alimtuma kwenda kujizamisha ndani ya mto wa Yordani. Hakuwa anajua wakati huo kwamba ukoma wake utaondoka. Taja vitu ambavyo hauwezi kufanya, kisha taja vitu ambavyo unataka, kama vile simu mpya au amani katika familia yako. Je, unaweza kufanya mambo ambayo hutaki ikiwa dhawabu yake ni kupata vitu unavyotaka?

## MCHEZO WA 3

**Hazina ya uwindaji**



Gawanya darasa kwa timu na uwe na mtoto mmoja kutoka kila timu ambaye atacheza wakati wenzake wanamshagilia mchezaji wa timu yao. Kwa kila timu, tayarisha bakuli au ndoo iliyojaa matope (au uji au kinamasi kingine chochote). Kuwa mwangalifu kuwa matope hayana vitu vikali ambayo vinaweza kuwajeruhi wachezaji. Katika kila ndoo ya matope, ficha idadi sawa ya klipu za karatasi au vifaa vingine vidogo kama "hazina" na mawe ili uifanye iwe sawa kwa kila timu. Unaposema "Nenda!" Kila mchezaji anatafuta ndani ya matope kwa kutumia

mkono wake ili apate klipu zote za karatasi anazoweza kupata katika sekunde 30. Toa muda zaidi kwa wachezaji wadogo. Fafanua kwa watoto kwamba matope yanawakilisha hali ngumu , klipu za karatasi zinawakilisha hazina ya uhusiano wa karibu na Mungu, na mawe inawakilisha ugumu wa moyo wa mtu.Ni jukumu la kila mmoja kutafuta hazina na kutojiruhusu moyo wake kujawa na machungu.




## MAHUDHURIO YA 3

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Ukoma**

## KAZI YA NYUMBANI 3

Sikiza ndugu zako wadogo, ndugu wadogo wa marafiki zako, au mtu ambaye kawaida huwa haumsikilizi. Jaribu kuelewa mtazamo wao. Ikiwa wanatambua kitu kibaya unachokifanya au kitu ambacho kinawafanya wasifurahie, wasikilize na ubadilishe tabia zako.

**Soma**

Siku ya 1: 2 Wafalme 18:1-9
Siku ya 2: 2 Wafalme 20:1-6
Siku ya 3: 2 Wafalme 20:7-11
Siku ya 4: Nehemia 1:1-6, 11
Siku ya 5: Nehemia 2:1-5



YEAH!!

# 4. CHUKUA HATUA KWA AJILI YA JAMBO



**Hadithi ya Bibilia: Hezekia na Nehemia**

2 Wafalme 18:1-8, 20: 1-11, 2 Mambo ya Nyakati 29:1-19, 29: 35-36, Nehemia 1:1–2: 5

## FUNGU LA 4 LA KUMBUKUMBU

Yohana 15:15 Siwaiti tena watumwa; kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki; kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu.



## HADITHI YA 4 YA UHITAJI

Barabara iliyo mbele ya nyumba ya Comet ilikuwa katika hali mbaya sana baada ya mvua na mashimo mengi. Ni mbaya sana kiasi kwamba hangeweza kuendesha baiskeli yake bila kuanguka ndani ya shimo. Aliamua kutengeneza kazi barabarani na kujaza mashimo yote kwa miamba na uchafu. Ilikuwa kazi ngumu sana kwamba nywele na nguo zake zote zilijaa uchafu. Watoto wa jirani walianza kumchekelea kwa kwa na sura zake iliyojaa uchafu.

## SOMO KUU LA 4

Leo tutaangazia Mashujaa wawili wa Imani. Kufikia sasa, tumejifunza zaidi jinsi ya kumtii Mungu na kumfuata na kumtafuta. Hayo ni mambo mazuri ambayo kuyatafuta kila wakati katika maisha yetu yote. Lakini Mungu hataki tumngoje Yeye atuambie tufanye vitu wakati wote (Zaburi 32: 9). Hakuna hata mmoja wa mashujaa wawili ambao tunawaangazia leo alisikia sauti ya Mungu au aliambiwa afanye kile alichofanya. Wote waliona hitaji na wakaamua kufanya kitu. Hezekia alikuwa mfalme akiwa na umri wa miaka 25, na alishuhudia jinsi Israeli ilivyokuwa imemkataa Mungu na kuruhusu hekalu iwe la hali mbaya. Jambo hili lilimsumbua, kwa hivyo alifanya uamuzi na kuwaongoza watu ili kusafisha na kukarabati hekalu. Alienda pia nchi nzima huku akaharibu sanamu zote, akiwaambia watu wamwabudu Mungu mmoja wa kweli. Vivyo hivyo, miaka mingi baadaye baada ya Israeli kuwa uhamishoni kwa muda mrefu, Nehemia alisikia kwamba ukuta wa Yerusalemu ulikuwa umeharibiwa na watu wameachwa hivyo. Mwanzoni, hakuwa kiongozi, lakini kitu kilimsumbua, na aliamua kuchukua hatua fulani kuhusu jambo hilo. Baada ya kusali na kufunga na kumtafuta Mungu, alimwomba mfalme wa Uajemi ruhusa na maandalizi ya kwenda Yerusalemu ili kurekebisha ukuta. Alikusanya Waisraeli wote walioishi Yerusalemu na akapanga ujenzi huo, licha ya upinzani kutoka kwa watu wa karibu.

Yesu alisema kwamba anataka tupendane na hivyo, kama marafiki wanaoelewa huduma Yake, anatuamini kuwa tutafanya mambo mazuri kwa ajili ya watu wake (Yohana 15: 12-17). Siku moja, ikiwa bado, utaweza kuanza kuwa na ndoto. Kunaweza kuwa na ukosefu wa haki ulimwenguni, kitu kinachokosekana kanisani, watu ambao wanapitia shida mtaani, watoto wanaohitaji makazi na familia, watu ambao hawajasikia kuhusu Mungu wetu wa ajabu na mwenye upendo, au watu wanaohitaji msaada. Je, ni nini hukupa wasiwasi? Je, nini hukufanya ulie na ukose usingize ukikiwaza? Labda sio wewe tu unayekuwa na wasiwasi huo, lakini Mungu pia ana wasiwasi na Yeye anakualika ujiunge na huduma Yake. Usisubiri tu maagizo, ingawa unapaswa kumtii Mungu ikiwa atakuambia usubiri. Vinginevyo, anza kuomba kwa ajili yake. Mwombe kwa ajili ya mafunzo unayohitaji na kwa ajili ya

usaidizi na mwongozo katika mradi huo. Tafuta watu wanaofanya jambo sawia la hilo na utafute njia za kujiunga nao. Ikiwa hakuna mtu anayefanya jambo kama hilo, basi kuwa wa kwanza!Usisubiri hadi utakapohisi uko tayari kwa sababu huwezi kuhisi uko tayari kabisa. Wala usidhani kuwa Mungu hawezi kukutumia sasa hata kama wewe ni mtoto (1Timotheo 4:12). Usijali kuhusu kile hauwezikufanya; angazia kile UNACHOWEZA kufanya na uanze mara moja!

Ninachagua kumwomba Mungu ili anisaidie kuchukua hatua kuhusu mambo yanayonipa wasiwasi ulimwenguni.


## SULUHISHO LA 4



Comet aliendelea kutengeneza barabara hadi ilipokamilika, akipuuza kicheko kutoka kwa majirani. Sasa sio yeye tu bali majirani wote wanaweza kutumia barabara vizuri bila matatizo kutoka kwa mashimo yote.

## SHUGHULI YA 4

**Udhalimu**



Fanya kila mtu aketi katika mduara na aweze kuhusu mambo yasiyo ya haki shuleni, kama vile mtoto ambaye huwa anasumbua wengine kila wakati, au watu wanapochukua vitu vyako bila ruhusa. Acha kila mtoto aseme jambo hata kama limeshasemwa. Sasa jadili kuhusu hatua inayopaswa kuchukuliwa, kama vile kumwambia mwalimu au mzazi, kuomba kwa Mungu ili akupe usaidizi, au kuonyesha huruma kwa wengine kama Mungu amekuonyesha rehema kwa dhambi zako.

## MSTARI WA 4 WA WAKATI

je, ni mwaka gani Hezekia alianza kutawala? Jibu: Karibu mwaka wa 715 K.K.

Je, Hezekia alifariki katika mwaka gani? Jibu: Katika mwaka wa 686 K.K. takriban

Je, ni mwaka gani ambao Nehemia alikarabati tena ukuta wa Yerusalemu? Jibu: Katika mwaka 444 K.K. takriban


## MAJIBU YA 4 YA MAFUMBO

### KWELI AMA UONGO

Weka mduara kwenye herufi hii ikiwa jibu ni kweli na kwenye herufi ikiwa jibu ni la uwongo.

1. Hezekia alikuwa mfalme akiwa na miaka 20.
2. Nehemia alijenga tena ukuta wa Yerusalemu peke yake.
3. Unaweza kuchukua hatuaa kuhusu jambo bila kusubiri yeyote akuombe.
4. Hezekia alitawala watu wa Israeli.
5. Wakati Nehemia alihisi wasiwasi baada ya kugundua ukuta umeharibiwa, alikuwa akiishi Uajemi.

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | K | U | T | A | S | I | N | A | M | I |
| I | P | P | E | H | E | K | A | L | U | E |
| A | Y | I | M | E | H | E | N | K | F | K |
| Y | P | N | L | A | I | R | A | E | O | I |
| P | A | Z | A | M | S | R | I | G | G | O |
| U | N | A | F | A | A | H | Z | N | A | N |
| A | G | N | M | B | D | S | A | A | M | G |
| G | A | I | A | S | U | H | U | R | N | O |
| N | R | T | I | R | A | T | A | H | T | Z |
| E | I | L | E | A | R | S | I | A | W | I |
| J | A | A | J | U | H | S | A | M | P | N |



## MASWALI NA MAJIBU 3

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, kuna jambo katika jamii au shule yako ambalo ni mbaya? Je, unaweza kuchukua hatua gani?
   (Kusudi hapa ni kuzungumza kuhusu ukosefu wa haki katika mazingira yao, na mambo ambayo wao wenyewe wanaweza kufanya ili kurejesha hali ili na usawa.) Mvulana ambaye anachekelewa shuleni, msichana mwingine ambaye hana chakula, au baba anayepiga mtoto wake kila siku. Zungumza kuhusu hatua wanazoweza kuchukua.
2. Je, Hezekia na Nehemia walichukua hatua, au walimtii Mungu tu?
   Jaribu kuwa na hoja, na usiseme tu ndio au hapana. Katika visa hivi 2 vya somo, unaweza kuona kwamba walishuhudia matatizo mawili na wakaamua kuchukua hatua ili kuirekebisha. Hakuna aliyepokea amri kutoka kwa Mungu, isipokuwa kile ambacho tayari kimechoandikwa katika bibilia. Walichukua hatua na kufanikiwa katika jambo kubwa kwa ajili ya Mungu.
3. Lakini je! Napaswa kujihusisha na biashara na matatizo ya watu wengine?
   Ongea kuhusu jinsi ya kuwajibika, na kwamba hatufai kuangazia mahitaji yetu tu. Unaweza pia kutumia hadithi ya Msamaria ambaye alisimama ili kusaidia badala ya kupita tu.




YEAH!!

## MCHEZO WA 4


**Wakazi wa nyumba**

Gawanya watoto katika vikundi vya 3. Watoto wawili katika kila kikundi wanaunda nyumba kwa kutumia miili yao ili kutengeneza kuta mbili na wakiinua mikono yao juu na kwa pamoja ili kuunda paa. Mtoto wa tatu anaingia ndani ya "nyumba" na anakuwa mkaazi. Wakati mwalimu anasema, "Mkazi!" Mkazi anatoka nje ya nyumba yake na kukimbia ili kutafuta nyumba zingine. Wakati mwalimu anasema, "Nyumba!" watoto wote wanaounda nyumba wanakimbia ili kuunda nyumba karibu na wakaazi tofauti.



## MAHUDHURIO YA 4

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:




**Nehemiya**

## KAZI YA 4 YA NYUMBANI

Angalia ulimwenguni wiki hii na upate jambo linalokupa wasiwasi. Omba Mungu ili asaidie watu wanaohusika, omba haki, amani na upendo. Kisha angalia ili upate njia fulani ambazo unaweza kusaidia, kama vile kutoa ushuhuda kuhusu jambo ambalo Mungu amekutendea hivi karibuni, kutoa mchango kwa shirika, kutoa mojawapo ya mali yako, au kutetea mtu kwenye uwanja wa michezo.

**Soma**

Siku ya 1: Esta 2:17-23
Siku ya 2: Esta 3:1-9
Siku ya 3: Esta 4:1-3, 12-17
Siku ya 4: Esta 5:1-8
Siku ya 5: Esta 5:9-14

# 5. KABILIANA NA HATARI



**Hadithi ya Biblia: Esta**

Esta 2-8

## FUNGU LA 5 LA KUMBUKUMBU

1 Wakorintho 15:58 Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana.

## HADITHI YA 5 YA UHITAJI



Taffy sasa ni kiongozi wa kikundi, na jambo hili linamfanya awe msichana maarufu zaidi darasani na wakati wote utawaona marafiki wakiwa wanamzunguka. Yeye anapenda kuchanganyika na kila mtu na kuwapa usaidizi. Siku moja "marafiki" zake walimshauri kuwa hapaswi kukaa na watoto wengine, kwa sababu walakuwa wanamfanya aonekane mbaya. Walimwambia kwamba yeye ni mtu wa kuheshimika sana na hivyo hapaswi kuingiliana na watoto ambao hakuna mtu anayewajali. Maneno haya yaliumiza sana moyo wa Taffy. Aliwaambia kuwa angeendelea kujumuisha kila mtu, kwa sababu alitaka kuwasaidia. Wakamjibu kwamba alipaswa ahague ikiwa alitaka kuwa nao au au watoto hao wengine, kwa sababu hawezi kuwa marafiki na wote hao.

## SOMO KUU LA 5

Leo tutaangazia mwanamke mwenye ujasiri ambaye alikabiliana na hatari ili kuokoa watu wake. Wayahudi (Waisraeli) walikuwa uhamishoni kwa sababu walikuwa wamempuuza Mungu. Lakini hata wakiwa uhamishoni, Mungu alitaka kuwasaidia. Mungu yupo pamoja nawe kila mahali uendako. Mfalme Xerxes wa Uajemi alimwondoa malkia kwa kutomtii mbele ya watu mashuhuri. Baadaye alitafuta malkia mpya, na mwanamke wa umri mdogo wa asili ya Kiyahudi aliyeitwa Esta akampendeza na kuwa malkia. Wakati huohuo, mtu mmoja aliyeitwa Hamani alipata madaraka na kuwa mtu wa karibu sana na mfalme. Hamani alimchukia Mordekai, binamu yake Esta ambaye alimlea. Alichukia hata Wayahudi wote katika ufalme wote. Kwa idhini ya mfalme, aliandika amri ya kumwambia watu waangamize Wayahudi katika siku fulani baadaye mwakani. Wayahudi wote walikuwa kwenye hatari kubwa! Wakamlilia Mungu awasaidie. Mordekai alimwomba Esta aende mbele ya mfalme na atetee maisha ya Wayahudi. Esta aliyekuwa mdogo aliingiwa na hofu, kwa sababu mtu yeyote ambaye alienda mbele ya mfalme bila kuitwa aliuawa.

Wiki iliyopita tulizungumza kuhusu mambo yanayokupa wasiwasi na jinsi unaweza kuchukua hatua kwa manufaa ya watu wa Mungu. Lakini itakuwaje ikiwa kuna uwezekani wa hatari na kuna nafasi kwamba mambo yanaweza kukugeukia na uumizwe kwa njia fulani? Esta alihatarisha kupata kifo ili kuokoa watu wake. Aliwaomba Wayahudi wote waombe na wafunge kula na kunywa pamoja naye na wenzake. Alipokaribia kwenye ukumbi wa mfalme, labda macho yake yalikwama kwa muda katika makali ya mapanga za walinzi. Inatisha sana! Lakini alikuwa tayari kuchukua hatua kwa ajili ya watu wake. Unapojawa na hofu, unaweza kumwomba Mungu kwa usaidizi. Unaweza pia kuchagua kuzingatia uwezekano wa matokeo mazuri mazuri badala ya kuwaza kuhusu matokeo mabaya, na kuamua kuwa mazuri yanayowezekana yanastahiki hatari zote. Mfalme alifurahishwa naye na akaja kwenye karamu

yake. Alimjulisha mfalme kuhusu njama ya Hamani, na hivyo mfalme akamwua Hamani. Lakini bado kulikuwa na tatizo! Tarehe bado ilikuwa imewekwa kwa kuuwa Wayahudi wote katika ufalme. Je, nini hutendeka ikiwa, wakati unachukua hatari, hakuna matokeo uliyotarajia? Je, unaacha na kukata tamaa?Ikiwa Esta angekata tamaa, Wayahudi wangekufa. Kwa ujasiri alirudi kwa mfalme tena, na wakatoa amri ya pili ambayo iliokoa Wayahudi wote.

Hatari inatisha kwa sababu haujui matokeo yake. Labda haitatendeka jinsi unavyotaka. Lakini haijalishi kitu kinatisha kwa jinsi gani, ujue mambo haya: Mungu yuko pamoja nawe wakati wote (Kumbukumbu la Torati 31:6, Mathayo 28:18-20). Yesu tayari ameshinda (Yohana 16:33). Mungu atabadilisha mambo mabaya kuwa mazuri kwa njia fulani (Warumi 8:28). Na hakika Mungu atakudhawabu (1 Wakorintho 15:58, Mwanzo 15:1).

Ninachagua kukabiliana na hatari na kumtafuta Mungu na wema kwa jili ya watu wake.



## SULUHISHO LA 5

Taffy aliamua kwamba kuwajali wengine ni muhimu zaidi kuliko kuwa maarufu. Alijibu marafiki hao kuwa hakujali kupoteza umaarufu na angeendelea kusaidia wale wanaomhitaji.

## SHUGHULI YA 5

**Ndovu aliyepakwa rangi**

Mchezaji mmoja ana jukumu la kuwa mwindaji katika upande mmoja wa chumba. Kwenye upande ule mwingine wa chumba, weka vifaa vya rangi mbalimbali. Mwindaji anasema jina la rangi, kisha wanafunzi wengine wote wanakimbilia ili kugusa kifaa kilicho na rangi hiyo. Mchezaji yeyote ambaye hatagusa kifaa cha rangi hiyo ndani ya sekunde 5 "anatekwa" na lazima aende aketi karibu na mwindaji. Kusudi la mwindaji ni kukamata wanafunzi wote. Mwalimu anaweza kuwa ndiye mwindaji katika zamu ya kwanza, kisha aruhusu wanafunzi wengine kubadilishana kuwa wawindaji.




## MSTARI WA 5 WA WAKATI

Je, Esta alitangazwa kuwa malkia katika mwaka gani? Jibu: Katika mwaka wa 478 K.K. takriban.

## MAJIBU YA 5 YA MAFUMBO

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| E | N | E | Y | U | K | Z | E | M | L | A | F | M |
| G | Y | A | H | I | M | N | H | N | A | A | T | O |
| J | O | G | H | A | M | A | N | I | N | A | E | R |
| L | N | D | O | G | T | U | R | N | Z | P | M | D |
| A | G | T | R | A | E | S | T | A | E | R | V | E |
| S | A | H | R | A | N | G | M | T | K | E | T | K |
| I | A | I | E | U | Q | I | A | I | Q | N | Y | A |
| R | S | H | C | W | E | N | R | S | P | V | G | I |
| I | P | E | A | M | C | A | R | H | L | S | R | K |
| S | A | R | U | G | E | S | T | A | O | Q | G | L |
| A | N | N | U | E | E | A | N | U | T | N | W | A |
| J | G | W | R | Z | V | H | T | W | Z | L | A | M |
| U | A | Y | P | L | O | D | H | K | S | O | R | D |





## MASWALI NA MAJIBU 5

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, tunapaswa kuchukua hatari kwa kiwango gani kwa ajili ya ufalme wa Mungu? Je, tunapaswa kuhatarisha ufadhili shuleni? Je, tunapaswa kuhatarisha kupoteza kazi, au hata kupoteza maisha yetu? Je, una maoni gani kuhusu mfano huu? Tuseme ndugu aanzishe kanisa katika mji na inakua kwa haraka na kufikia watu 400. Mchungaji anaamua kuchukua hatari na benki na anatumia jengo ili kuanzisha kanisa lingine katika mji jirani. Ikiwa atafanikiwa, atakuwa na makanisa 2 mazuri. Ikiwa hatafanikwa, anahatarisha kupoteza jengo 1 ambalo tayari analo. Je, ni vizuri kujihatarisha kwa ajili ya ufalme wa Mungu kwa kiwango kama hicho?
   Usiruhusu wanafunzi watoe majibu ya haraka. Jambo la muhimu ni kwamba wanajadili kuwa kuna hatari kubwa maishani, na kwamba wakati mwingine hatari hizo huwa ngumu sana.
2. Je, sote tunapaswa kuchukua hatari katika maisha yetu?
   NDIYO! Ni muhimu kwamba wanafunzi waelewe kuwa Mungu aliumba ulimwengu na maisha ya Kikristo na yakiwa na HATARI kama sehemu muhimu. Sababu ni kwamba kulingana na Mungu, IMANI ni muhimu sana. Mungu anajali


zaidi kuhus ya imani yetu katika kuamini kile Mungu anatuomba tufanye, kuliko thamani ya jengo. Lazima Sote tuchukue hatari kwa ajili ya Mungu.


3. Je, umechukua hatari gani?
   Wape wakati wa kuwaza na kushuhudia maisha yao ya kibinafsi. Haijalishi ikiwa ni jambo ndogo. Sote tunapaswa kuanza na jambo ndogo.

## MCHEZO WA 5

**Mashindano ya mpira ya karatasi iliyokunjwa**

Kwenye karatasi kubwa, chora lengo na miduara 3. Mduara wa kati una thamani ya alama 100, unaoufuata una alama 50, na mduara wa nje una alama 10. Kisha watoto wanatakiwa kukunja vipande vidogo vya karatasi kuwa mipira ndogo na kujaribu kugonga lengo kwa kurusha karatasi kwa vinywa vyao. Vinginevyo, wanaweza kurusha mipira ya karatasi kupitia majani ymrija wa kunywa.






## MAHUDHURIO YA 5

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Esta**

## KAZI YA 5 YA NYUMBANI

Muombe Mungu akupe fursa ya kufanya jambo nzuri kwa ajili yake wiki hii, kama vile kuhubiria mtu kuhusu Yesu, kuomba kwa sauti katika kikundi, au kuzungumza na mtu mpya. Wakati muda huo utakapofika, ikiwa una hofu ya kufanya, waza kuhusu jinsi jambo hili linaweza kuwa baraka kwa mtu huyo mwingine na ujaribu kulifanya. Ukikosa kufanikiwa mara ya kwanza, ni sawa. Muombe Mungu akupe usaidizi na ujaribu tena na tena hadi ufanikiwe.

**Soma**

Siku ya 1: Ayubu 1:1-5
Siku ya 2: Ayubu 1:6-12
Siku ya 3: Ayubu 1:13-22
Siku ya 4: Ayubu 2:1-10
Siku ya 5: Ayubu 2:11–3: 4

# 6. HAZINA ILIYOFICHWA



**Hadithi ya Bibilia: Ayubu**

Ayubu 1:1-3:4, 40:1-14, 42

## FUNGU LA 6 LA KUMBUKUMBU

Isaya 55:9  Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.

## HADITHI YA 6 YA UHITAJI



Kip alipenda kumtumikia sana Mungu kanisani, pia shuleni alizungumzia na kuimba kuhusu Mungu. Alikuwa na wanafunzi wenzake darasa ambao hawakupendelea alipofanya hivyo na hivyo wakaanza kumuudhi. Walikuwa wakichuka penseli zake, madaftari yake, hata siku moja waliiba mfuko wake. Wakamshutumu kwa mambo ambayo hajafanya, na mkurugenzi wa shule hiyo alimwagiza afike simu ofisini yaake, akaadhibiwa kwa jambo ambalo hakufanya.

## SOMO KUU LA 6

Leo tutaangazia hazina fulani ambayo imefichwa sana kiasi kwamba watu wengi huwa hawaitafuti. Shujaa wa Leo wa Imani, Ayubu, alikuwa mwadilifu kiasi kwamba Mungu akamweleze Ibilisi kumhusu Je, inaweza kushangaza kwa namna gani ikiwa Mungu angesema jambo kukuhusu, "Kila mtu, angalieni jinsi mwana/binti yangu alivyo"? Ibilisi alisema kwamba alikuwa na sifa hizo kwa sababu ya baraka tu. Mungu alimpa ibilisi ruhusa ya kumjaribu Ayubu kwa kuondoa mali yake yote na hata wanawe na binti zake. Mungu ana mamlaka yote katika ulimwengu kiasi kwamba hata adui hawezi kufanya chochote bila idhini ya Mungu. Ayubu alitenda kwa njia ya haki, kwa hivyo kwa idhini, ibilisi alimpa ugonjwa wenye uchungu. Katika hadithi hii, Mungu alituonyesha jinsi mambo yalivyo mbinguni kwa uhalisi.

Marafiki wa Ayubu walikuja na kumwambia kwamba maumivu yake yalitokana na uovu wake. Ayubu alidhani alikuwa mwadilifu na kwamba kahustahili maumivu. Kwa njia hiyo hiyo, watu wengine hudhani wanapaswa kuwa na maisha mema wakati wote kwa sababu wanamfuata Mungu. Mwisho wa hadithi, tunaona hazina ambayo Ayubu alipokea. Mungu mwenyewe alizungumza na Ayubu moja kwa moja! Iwe Ayubu alimuona Mungu au alielewa tu sauti Yake, lakini alishangaa kabisa. Aliona kuwa Mungu ana mamlaka juu ya ulimwengu wote: nyota na viumbe na ngurumo kubwa na volkeno kubwa na vitu vyote vinavyotuzunguka. Alinyenyekea na kukubali kwamba hekima ya Mungu ni zaidi ya uelewa wa mwanadamu. Baadaye, Mungu alimbariki Ayubu na utajiri na wana na binti hata zaidi, lakini wakati huu Ayubu tayari amebadilisha mtazamo wake na alikwa na ujuzi bora kuhusu Mungu.

Kwenye dunia hii kuna maumivu. Wakati mwingine shetani ana ruhusa kutoka kwa Mungu ya kutujaribu kama Ayubu. Wakati mwingine mambo mabaya hufanyika kwa sababu tu ulimwengu huu umeharibiwa na dhambi. Na wakati mwingine Mungu anatuomba tufanye jambo ambalo husababisha maumivu kwa muda. Mungu alimwomba Mwanawe Yesu apitie kifo chenye uchungu msalabani. Tena, Mungu alituonyesha jinsi mambo yalivyo kwa uhalisia. Usiku kabla ya Yesu kusulubiwa, Aliuliza Baba Mungu ikiwa kuna njia nyingine; lakini bado alisalimisha kwa mapenzi ya Mungu (Mathayo 36-39). Yesu anafahamu yale tunapitia (2 Wakorintho 1:5). Haijalishi maumivu yanatoka wapi, tunaweza kumtafuta

Mungu katikati ya tatizo lenyewe na tukubali kuwa hekima ya Mungu inashinda uelewa wetu (Isaya 55: 9). Kama vile Mungu alivyotumia mateso ya Yesu ili kuokoa ulimwengu wote, Mungu anaweza kutumia hali yako yenye uchungu ili kubariki watu wengi karibu nawe kwa njia fulani. Lakini unaweza kupata hazina kubwa mara moja. Mungu yuko karibu na waliovunjika mioyo (Zaburi 34:18), na unapomtii Mungu katika maumivu yako, anaweza kuwa karibu nawe hata zaidi.Ingawa maumivu ni ya muda mfupi, hazina kubwa zaidi katika ulimwengu wote - uhusiano wa karibu na Mungu - utadumu milele na milele!

Ninakiri hekima ya Mungu inashinda uelewa wangu na ninachagua kumtafuta Mungu hata katika uchungu.




## SULUHISHO LA 6

Hata katika hali hii aliendelea kumsifu Mungu na kuwaombea wenzake.

## SHUGHULI YA 6

**Kitu cha thamani**

Kila mtoto anaandika au anachora vitu tofauti ambavyo anachukulia kuwa vya thamani maishani mwao,  kama vile wazazi, marafiki, Mungu, shule, nk. Baada ya hapo, waulize watoto wajadili na mwanafunzi 1 au 2 kuhusu michoro yao na kujadili kwa nini wanachukuli kuwa hio ni hazina kwao.




## MSTARI WA 6 WA WAKATI

Je, hadithi ya Ayubu ilitokea katika mwaka gani? Jibu: Hatujui haswa, kwa sababu hakuna tarehe iliyoonyeshwa katika Bibilia. Inakadiriwa kati ya 2200 K.K. na 1520 K.K.

## MAJIBU YA 6 YA MAFUMBO

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | Y | U | B | U | I | N | A | T | E | H | S |
| U | H | U | S | I | A | N | O | S | S | I | U |
| U | G | O | N | J | W | A | A | F | L | N | T |
| M | F | V | D | D | I | I | L | U | U | A | A |
| A | R | I | K | I | H | S | F | A | O | H | J |
| S | I | D | N | T | K | I | I | N | V | I | I |
| K | E | O | E | I | L | I | H | L | U | T | R |
| I | S | N | E | I | M | E | F | A | I | M | I |
| N | T | D | D | F | D | A | K | A | K | B | S |
| I | T | A | E | R | U | S | A | A | R | I | I |
| L | W | H | A | Z | I | N | A | W | E | A | A |
| M | N | Y | E | N | Y | E | K | E | V | U | M |





## MASWALI NA MAJIBU YA 6

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, Mungu anaweza kuruhusu jambo mbaya linitendekee ili kunijaribu?
   NDIYO! Jinsi tulizungumza katika masomo ya awali, Mungu anajali zaidi maisha yetu ya kiroho kuliko maisha yetu ya mwili. Ikiwa tunaweza kushinda mtihani vizuri, na tupate alama nzuri kutoka kwa Mungu mwenyewe, na sio kulalamika, tutakuwa tumeshinda! Mungu ametuonyesha kuwa hili ni muhimu zaidi kwake kuliko mali zetu, familia zetu, na hata maisha yetu. Sababu ni kwamba hatuko hapa duniani kwa muda mrefu. Maisha ya milele ndio jambo muhimu.
2. Je, ikiwa kila mtu shuleni anaiba mitihani na anapata alama nzuri kila wakati, ninawezaje kupita jaribio hili?
   Kama jinsi Ayubu alivyofanya, kuvumilia alama mbaya, ingawa hali ni ngumu, bila KULALAMIKA! Kama hatutaki kushinda jaribio, tutakata tamaa na tuanze kuiba pia.
3. Je, mambo mabaya ambayo huwafanyika watu yanahusiana moja kwa moja na dhambi?
   Bibilia ina mfano wa pande zote. Hapa, katika mfano wa Ayubu, jibu ni HAPANA. Ayubu hakufanya dhambi ili astahili mambo mabaya. Lakini kuna hali katika Bibilia ambapo tunaona jibu ni NDIYO. Kwa mfano, mji wa Sodoma na Gomora. Mungu anatuambia katika Bibilia ya kwamba mji huo ulichomwa kwa sababu ya dhambi ndani yake. Jibu wakati mwingine huwa ndiyo, na wakati mwingine huwa hapana. Mungu ametuambia tusiwahukumu wengine na kwamba ikiwa tuna rehema, pia sisi tutapokea rehema kutoka kwake. Usijaribu kuhusisha maumivu ya mtu mwingine na dhambi zake kwa sababu haujui kile Mungu anafanya katika maisha yao. Labda wana bahati nzuri, kwa sababu Mungu anaichukulia mioyo yao kuwa ya thamani vya kutosha ili kupitia maumivu wanayopata.

## MCHEZO WA 6


**Mawindo ya Mkangaji**

Kusanya vifaa vidogo au vichezeo na uvifiche. Ikiwa unaweza kucheza nje, vifiche kwenye kichaka au mimea. Ikiwa unacheza ndani, vifiche chini ya meza, viti, au chini ya mikeka kwenye chumba. Andaa orodha ya vitu vyote vilivyofichwa kwa kila mchezaji. Unaweza kupanga watoto kulingana na timu au jozi. Watoto wanapaswa kuacha kifaa mahali walipokipata lakini lazima wakumbuke mahali kilikuwa. Mshiriki au timu ya kwanza kupata vitu vyote inashinda.



## MAHUDHURIO YA 6

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:




**Ayubu**

## KAZI YA 6 YA NYUMBANI

Waza kuhusu hali mgumu katika maisha yako hivi karibuni. Je, hali hii ilisababisha matokeo gani mazuri? Inaweza kuwa ngumu kuvitambua, lakini unaweza kumwomba Mungu akusaidie utambue mambo mazuri ambayo Mungu alifanya kupitia hali hiyo Kisha andika au uchore picha za mambo yote mazuri na umshukuru Mungu kwa hilo. Waambie wazazi wako na mwalimu wako kuhusu hali hio.

**Soma**

Siku ya 1: Isaya 52:1-4
Siku ya 2: Isaya 52:5-10
Siku ya 3: Isaya 52:11-15
Siku ya 4: Isaya 53:1-6
Siku ya 5: Isaya 53:7-1

# 7. MATUMAINI YA MAMBO MAZURI



**Hadithi ya Bibilia: Isaya**

Isaya 6:1-8, 9:6-7, 42:1-4, 53, 65:17-19

## FUNGU LA 7 LA KUMBUKUMBU

2 Wakorintho 5:20 Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu.

## HADITHI YA 7 YA UHITAJI



Wazazi wa Peppy walikuwa wamekwenda safarini, na wakamuahidi yeye na nduguze kuwapa thawabu nzuri ikiwa watakuwa na tabia nzuri.Ndugu zake walimwambia Peppy kwamba wanaweza kufanya chochote wanachotaka kwa sababu walikuwa peke yao. Peppy aliwaambia kwamba alitaka kufanya mambo mazuri tu, ili wazazi wake watakaporudi, wampe tuzo nzuri. Ndugu zake walimwambia hilo haliwezekani, na kwamba wazazi wataleta kila mtu kitu kizuri. Peppy akawajibu kuwa aalifahamu hilo na kwamba wangeleta zawadi nzuri. Akataa kufanya mabaya na hakufuata ndugu zake walipokuwa wakifanya mambo mabaya.

## SOMO KUU LA 7

Katika somo la leo la Mashujaa wa Imani, tutaangazia nabii ambaye alikuwa na kazi maalum sana. Wacha tuangalie jinsi Mungu alivyomwita Isaya kama nabii. Isaya aliona maono ya ajabu ya mbinguni (Isaya 6). Unapoendelea kutumia wakati wako na Mungu kila siku, unapofuata na kumtii Mungu kwa kila sehemu ya maisha yako, utaelewa zaidi na zaidi jinsi Mungu wetu alivyo mtakatifu na wa kushangaza. Na kama Petro, jinsi alivyotambua Yesu alikuwa nani na kutambua dhambi yake mwenyewe (Luka 5: 8), unapotambua utakatifu wa Mungu, utaweza kuona vyema zaidi dhambi yako na udhaifu wako mwenyewe. Lakini usiwe na wasiwasi! Katika maono ya Isaya, malaika aligusa midomo yake na kusema ilikuwa safi. Kwa njia hiyo hiyo, Yesu anakuita msafi, sio kwa sababu ya mambo uliotenda lakini kwa sababu ya kile alichotenda (Yohana 15: 3). Kisha katika maono, Mungu aliuliza ni nani angeweza kutuma, na Isaya akasema, “Nichague! Nitume!" Leo, pia, Mungu anaangalia duniani kote ili kuona ni nani aliyejitolea kikamilifu kwa ajili yake (2 Mambo ya Nyakati 16:9) na ni nani anayeweza kumtuma kwa niaba yake. Unaweza kumwambia akuchague! Umetumwa na Mungu ili kumwakilisha katika ulimwengu huu, na kuhimiza watu ili wamfuate (2 Wakorintho 5:20).

Isaya alikuwa na kazi ya kushangaza! Ikiwa utamwomba Mungu akuchague, anaweza kuwa na vitu vya kushangaza ajili yako, pia. Isaya aliweza kuwa na fursa ya kutabiri kuhusu kuja kwa Yesu. Mungu alimwonyesha siku za baadaye zenye matumaini kwa Israeli na kwa ulimwengu wote.

Karibu miaka elfu baadaye, mwanafunzi anayeitwa Filipo alikutana na Mtowashi Mhabeshi ambaye alikuwa akisoma kitabu hiki hiki cha Isaya ambacho tunasoma siku ya leo. Alisoma unabii huo katika

Isaya 53:7, na Filipo alipomfafanulia, Mtowashi huyo alimkubali Yesu! Kwa hivyo, pia wewe, unapoomba Mungu akutume kama Isaya, Mungu atatenda mambo makuu kupitia wewe. Lakini tunapoangalia mazingira yetu, tunaweza tu kuona eneo ndogo linalotuzunguka na wakati mdogo wa maisha yetu. Wakati Mungu anaangalia mazingira yaek, Anaona ulimwengu wote na wakati wote kabla na baada yetu. Anapanga kila aina ya mambo ya ajabu ambayo yanaweza kuanza unaposema "ndiyo" yako rahisi .Lakini hautajua ukubwa wa yale Mungu alifanya kupitia wewe hadi utakapofika mbinguni, ambapo labda utashangaa sana kuona jinsi Mungu alivyondelea kukutumia muda mrefu baada ya kuondoka kutoka duniani.

Na tukizungumzia mbingu, Isaya aliendelea kutazamia mema, mbali na siku zijazo. Mungu alimpa kazi ya kutabiri sio tu kuhusu Yesu lakini kuhusu mbingu vile vile. Je, utamwomba Mungu akuchague na akutumia ili kuleta matumaini katika ulimwengu kwa kuwaelekeza watu kwa Yesu na kuwasaidia kutazamia mbinguni pia?

Ninachagua kumwomba Mungu anichague na kutazamia wakati ujao katika siku zijazo.




## SULUHISHO LA 7

Mwishowe alipokea thawabu aliyotarajia.

## SHUGHULI YA 7

**Mafumbo pamoja na muziki**

Tayarisha kabla ya wakati vipande vya karatasi vilivyo na maandishi ya nyimbo tofauti. Kulingana na umri katika darasa lako na ugumu wa muziki, tenga maandishi kulingana na kila neno au kulingana na aya na uweke vipande kwenye mifuko. Ili kucheza, gawanya darasa lako kwa timu na upe kila timu mfuko. Cheza muziki kwa ajili yao, na timu ya kwanza kuweka pamoja maandishi ya wimbo inashinda. Mchezo huu pia unaweza kutumika vizuri ili kukagua mafungu ya kumbukumbu ya awali.



## MSTARI WA 7 WA WAKATI

Je, Isaya alizaliwa lini? Jibu: Katika mwaka wa 766 K.K. takriban

Je, Isaya alifariki lini? Jibu: Katika mwaka wa 686 K.K. takriban

## MAJIBU YA 7 YA MAFUMBO

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| E | K | I | L | I | J | N | I | A | Z | E | N | E | U | K |
| E | U | R | F | K | R | O | W | E | Z | R | E | S | K | A |
| T | J | A | E | S | A | M | F | S | K | D | T | N | Y | I |
| A | I | N | I | A | M | U | T | A | M | U | T | A | P | K |
| I | T | O | S | F | O | I | Z | E | E | A | S | I | H | I |
| B | O | H | Q | U | K | I | Z | U | R | I | O | S | I | M |
| M | L | S | I | K | U | Z | I | J | A | Z | O | N | L | U |
| A | E | I | H | S | I | L | I | K | A | W | M | V | O | T |
| U | A | M | A | S | O | P | I | L | I | F | A | W | U | U |
| K | F | M | H | A | B | E | S | H | I | D | N | D | A | K |

| * | / | . | ; | [ |
|---|---|---|---|---|
| 54 | 35 | 40 | 25 | 39 |

| } | " | ] | ° | ! |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 16 | 10 | 11 | 10 |



## MASWALI NA MAJIBU YA 7

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**


1. Watu wanasema au kutangaza ahadi za Mungu. Lakini tunawezaje kutambua ni zipi ambazo ni za kweli na uwongo? Tunafanya nini?
   Zungumza na wanafunzi kuhusu tofauti kati ya kutangaza kuwa utapata gari mpya nyekundu dhidi ya kuamini kuwa Mungu atakupa kazi. Pia jadili kuhusu ahadi ambayo pengine Mungu alikueleza au ahadi iliyoandikwa katika Bibilia. Kwa mfano, "Mungu atatenda jambo nzuri maishani mwangu hata ingawa mambo mabaya yanatendekea kwa sasa." Kwa upande mwingine, Mungu sio mashine ya mauzo ambapo unaweka dola 1 na kitu tunachotaka kinatokea.
2. Je, kuna wakati ambapo uliamini kwamba Mungu angefanya kitu kisha akakifanya?
   Wape wanafunzi muda wa kushiriki. Itakuwa vyema utayarishe shuhuda zako mapema, ili mawazo yatiririka.
3. Je, tunahitaji kusubiri kwa muda gani na kutumainikuwa mazuri yatatendeka?
   Waache wazungumze kuhusu majibu kuuazia kusubiri saa 1 hadi miaka. Wakumbushe kwamba Isaya alitabiri kuhusu Masiya, na unabii wake ulikuwa sahihi, ingawa hakuweza kumwona wakati wa maisha yake. Wakati mwingine hatutaweza kushuhudia mazuri yakitimizwa wakati wa maisha yetu. Lakini Mungu hashindwi.



YEAH!!


## MCHEZO WA 7

**Mchoro wa kipofu**



Gawanya darasa kwa jozi. Katika kila jozi, funga macho ya mchezaji mmoja na uwape karatasi na penseli.  Mchezaji huyo mwingine atasoma neno unaloandika ubaoni au kulisema kimya kimya kwa mwenzake aliyefungwa macho na atamwelekeza lichore bila kusema lolote. Kwa mfano, ikiwa utaandika "nyumba", mwelekezi sio lazima aseme nyumba kwa maneno lakini lazima amwelekeze mwenzake ili achore mstatili na pembetatu juu kama ilivyo nyumba, nk.

## MAHUDHURIO YA 7




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Isaya**

## KAZI YA 7 YA NYUMBANI

Kila wakati jambo nzuri linapotokea wiki hii, fikiria jinsi mbinguni itakuwa bora hata zaidi. Wakati wowote kitu kibaya kitapokea, kumbuka jinsi Mungu atafuta machozi yote mbinguni. Bonasi, fanya hii tu ikiwa unataka: muombe Mungu akuchague na akutume. Hili ni jambo lenye uzito sana. Ukimwomba, atakuchagua na kukutumia, na hakuna kurudi nyuma.

**Soma**

Siku ya 1: Yeremia 1:9-14
Siku ya 2: Yeremia 20:3-6
Siku ya 3: Yeremia 20:7-12
Siku ya 4: Yeremia 20:13-18
Siku ya 5: Yeremia 37:11-17

# 8. VUMILIA UPINZANI



**Hadithi ya Bibilia: Yeremia**

Yeremia 1:4-19, 15:15-21, 26:7-16, 37:11-21, 38:6-10, 39:1-2, 39:11-12

## FUNGU LA 8 LA KUMBUKUMBU

Matendo 4:29 Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote,



## HADITHI YA 8 YA UHITAJI

Wakati walikuwa wakiomba, Buzz alihisi sana kwamba Mungu alikuwa anamtaka azungumze na watoto walio eneo la karibu kuhusu Neno la Mungu. Hakuwa na uhakika sana na hili, kwani walikuwa kwenye eneo jipya. Lakini sauti ilikuwa inaendelea kuongezeka. Aliamua kuifanya hivyo, lakini kila wakati alipozungumza na mtu, walimcheka, na hilo lilimfanya ahisi huzuni kidogo.

## SOMO KUU LA 8

Karibu tena katika Mashujaa wa Imani! Leo tutaangazia mtu ambaye alikabiliwa na upinzani maishani yake yote na ambaye Mungu alimpa nguvu. Yeremia aliishi wakati wa wafalme wa mwisho wa taifa la Yuda

Mungu alimwita Yeremia akiwa na umri mdogo. Mungu alimwambia Yeremia kwamba alimjua hata kabla ya kuwa tumboni mwa mamake. Mungu alikujua kabla hata ya uwepo wako, pia! Na Mungu amekutenga ili ufanye mambo ambayo amekuandalia. Mpango wa Mungu juu ya maisha ya Yeremia ulikuwa awe nabii, aongee kwa niaba ya Mungu kwa mataifa. Mungu alimwambia kwamba atampa nguvu, kama ukuta wa shaba. Ujumbe wa Yeremia katika maisha yake yote ulikuwa ni kuambia watu Yuda waache kumuacha Mungu wao, na kwamba Mungu angewatuma uhamishoni Babeli. Watu walipuuza Yeremia na kumpinga maisha yake yote.

Wakati mmoja, Yeremia alivunjika moyo. Alitazama mazingira yake na kuona tu mambo yaliyokuwa yakitendekea karibu naye, hakuona jinsi Mungu alimwinua. Ni rahisi sana kuanza kulalamika wakati mambo yanaonekana kuwa mabaya na kusahau Mungu anayekutunza. Mungu alimwambia atubu na akamhakikishia kwamba atamwokoa. Mungu alimwambia tena ajikaze na asifuate njia za kila mtu aliye karibu naye.

Yeremia alivumilia upinzani mwingi. Wakati mmoja walitishia kumuua Yeremia kwa sababu ya maneno aliyozungumza. Yeremia alitupwa ndani ya tangimaji kwa muda, kisha akafungwa gerezani. Ingawa alikuwa akizungumza kwa niaba ya Mungu, walimshtaki kuwa ni mpelelezi wa Babeli. Kama vile Yeremia alivyoshutumiwa kwa uwongo, ndivyo pia Yesu alishtumiwa alipozungumza kwa niaba ya Mungu. Siku zote kuna watu ulimwenguni wanaokataa maneno ya Yesu, na watakataa maneno yetu, pia. Baada ya Yesu kwenda mbinguni, wanafunzi walihubiri neno la Mungu kwa wazi na watu wengi walimfuata Yesu. Baadaye, walikabiliwa na upinzani na walipigwa viboko na kufungwa. Badala kuvunjika moyo, kama

Yeremia, walimgeukia Mungu kwa ujasiri wa kuendelea kuhubiri neno la Mungu licha ya upinzani (Matendo 4:29). Unaweza kumuuliza Mungu akupe ujasiri pia.

Baada ya miaka mingi ya kutabiri kuhusu uhamisho, maneno ya Yeremia yalitimia. Wababeli walikuja na kushinda Yerusalemu, wakavunja kuta zake na wakaiteketeza. Walichukua watu wengi na kuwapeleka Babeli.Lakini Mungu hakuwahi kuwaacha watu wake. Alizungumza kupitia Yeremia, akisema kwamba Mungu alikuwa amewatuma watu waadilifu huko Babeli na atakuwa pamoja nao (Yeremia 24:5-7). Tutashuhudia hayo katika masomo yanayokuja katika Mashujaa.

Wababeli walipodhibiti Yerusalemu, walimwachilia huru Yeremia. Mungu alimuokoa jinsi tu alivyokuwa ameahidi. Kama Isaya kwenye somo la mwisho, Yeremia hakujali kuhusu ulimwengu huu lakini alitazamia mbingu mpya ya Mungu (Waebrania 11: 13-16).

Ninachagua kutetea ukweli wa Mungu na kuzungumza kuhusu neno la Mungu na kuvumilia upinzani.


## SULUHISHO LA 8



Lakini Mungu aliendelea kuzungumza naye, kwa hivyo akasimama kidete bila kujali alichoambiwa, aliendelea kuhubiri Neno, kwa sababu alijua Mungu alikuwa pamoja naye.

## SHUGHULI YA 8

**Kila kondoo na jozi lake**




Mwalimu anasema sheria tofauti, na watoto lazima wajipange katika kundi ipasavyo. Kwa mfano, mwalimu anasema "mashati meupe dhidi ya mashati ya rangi" na watoto wote wenye mashati meupe wanaenda upande mmoja wa chumba wakati watoto wote waliovaa mashati ya rangi wanaenda upande wa pili. Sheria zingine zinaweza kuwa nywele ndefu dhidi ya nywele fupi, au siku za kuzaliwa kuanzia Januari - Juni dhidi ya Julai - Disemba, kati ya wasichana sheria inaweza nywele zilizofungwa dhidi ya nywele huru na kulingana na umri au eneo unaweza kusema suruali fupi dhidi ya suruali ndefu. Unaweza pia kuweka sheria ya mgawanyiko pamoja na shughuli ambayo unataka kuendeleza.


## MSTARI WA 8 WA WAKATI

Je, Yeremia alizaliwa katika mwaka gani? Jibu: Katika mwaka wa 643 K.K. takriban

Je, Yeremia alikufa katika mwaka gani? Jibu: Katika mwaka 570 K.K. takriban

## MAJIBU YA 8 YA MAFUMBO







## MASWALI NA MAJIBU 8

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Maisha ya Mkristo ni rahisi, au sivyo? Na waumini wanalindwa na Mungu kila wakati, au sivyo?
Kwa kweli Mungu anatulinga, lakini haimaanishi kuwa maisha yatakuwa rahisi. Kama tulivyoshuhudia kwenye somo, tunaweza kubabiliwa na adhabu za kusingiziwa na kudhihakiwa, hata kufungwa gerezani, lakini haijalishi. Mungu ataruhusu yote haya, kwa sababu kulingana na Mungu, maisha yetu ya kiroho ni muhimu zaidi kuliko ile ya mwili. Labda jambo kubwa kwa ajili ya nchi ni muhimu zaidi, ambalo linajumuisha jambo ngumu zaidi kwa Wakristo wanaoishi huko.

2. Je, unapaswa na angalau umri gani ili kupokea mwito wa Mungu katika huduma?
Yeremia aliitwa wakati fulani akiwa na kati ya miaka 10 na 17. Zungumza na wanafunzi wako kuhusu ukweli kwamba SASA HIVI Mungu anaweza kukuita!




YEAH!!


3. Je, kuna aina gani ya upinzani leo shuleni?
Zungumza kuhusu njia tofauti ili uwasaidie wanafunzi kuelezea kila kitu wanachohitaji kuvumilia. Mfano: mtu anachukua chakula chako, mwalimu anakupa alama mbaya, baba yako anapoteza kazi, hakuna mtu anayecheza na wewe wakati wa mapumziko, mvulana akishambulia barabarani ukielekea nyumbani baada ya shule, nk.

## MCHEZO WA 8

**Uwindaji wa Puto**



Toa kwa kila mchezaji puto iliyojazwa pumzi na uifunge kwenye kifundo cha mguu wao kwa kutumia kamba Hakikisha kuwa puto zote zimejazwa pumzi kwa kiwango sawa. Lengo la mchezo ni kutoboa puto za wachezaji wengine kwa kutumia miguu pekee na kuzuia wengine wasitoboe puto yako. Weka muda au cheza muziki fulani, na muda unapokwisha, mtu yeyote ambaye puto yake bado haijatobolewa anashinda.




## MAHUDHURIO YA 8

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Yeremia**

## KAZI YA 8 YA NYUMBANI

Soma Bibilia kila siku wiki hii, hata kama ni kwa dakika chache tu. Kitabu cha Yohana au Zaburi ni vitabu rahisi sna vya kuanza. Ikiwa huwezi kusoma, muombe mtu akusomee kidogo. Ikiwa umekosa kusoma katika siku fulani, usisumbuke sana kutokana na hilo. Jaribu tena siku inayofuata. Ikiwa umweza kusoma Bibilia kila siku, hongera! Endelea kuisoma.

**Soma**

Siku ya 1: Danieli 3:1-6
Siku ya 2: Danieli 3:7-12
Siku ya 3: Danieli 3:13-18
Siku ya 4: Danieli 3:19-25
Siku ya 5: Danieli 3:26-30

# 9. LIPA GHARAMA



**Hadithi ya Biblia: Shadraka, Meshaki na Abednego**

Danieli 3

## FUNGU LA 9 LA KUMBUKUMBU

Waebrania 11:16 Lakini sasa waitamani nchi iliyo bora, yaani, ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea mji.

## HADITHI YA 9 YA UHITAJI



Taffy alikuwa mwanafunzi mwerevu zaidi darasani. Siku moja mwalimu aliwwomba afanye mradi nyumbani kwa ajili ya sherehe. Sherehe hii ilikuwa kinyume na maandiko ya biblia. Taffy alipogundua kuwa kile mwalimu alikuwa amemwomba kilikuwa kinyume na imani yake, alimweleza mwalimu kwamba hangweza kushiriki kwa sababu haikuwa sawa kwake. Mwalimu alitishia kwamba ikiwa hatatekeleza jukumu hilo, angempa alama za chini.

## SOMO KUU LA 9

Wiki iliyopita tulishuhudia jinsi watu Yuda walivyoenda uhamishoni Babeli. Leo tutaanza kuona jinsi Mungu aliendelea kuwa nao. Vijana watatu wa Kiyahudi walioitwa Shadraka, Meshaki na Abednego walipelekwa Babeli na walipewa kazi ya kusimamia mkoa katika Babeli. Mfalme aliamua kuweka sanamu kubwa na kuwaamrsiha viongozi wake wote waiabudu, vinginevyo watatupwa katika tanuru kwa kutotii. Watu wanadhani wakitutishia wanaweza kubadilisha imani yetu. Hawatarajii kwamba tuko tayari kulipa gharama. Lakini tofauti na miungu yao, Mungu wetu tayari anatuongoza na ametulipia gharama, na tunaweza pia kufurahia kwa kila fursa ya kufanya vivyo hivyo kwa ajili ya Mungu.

Shadraka, Meshaki, na Abednego walichagua kuendelea kuwa waaminifu kwa Mungu wao na kulipa gharama. Walijua Mungu ana uwezo wa kuwaokoa, lakini hawakuwa wanakujua ikiwa Mungu angewaokoa duniani au mbinguni. Walinzi waliwatupa katika tanuru pamoja na nguo na kila kitu, ingawa nguo zilikuwa za thamani sana. Leo, watu wanapokataa maneno ya Yesu, wanaweza hata kukataa mambo yote mazuri ambayo Mungu amekutendea, pia, kama vile walivyokataa miujiza ya Yesu na mamlaka ya Mungu ndani yake (Mathayo 12:24). Lakini maoni yao haijalishi kwa sababu cha muhimu zaidi ni maoni ya Mungu kuhusu maisha yako. Kazi hizo zote nzuri Anazofanya kupitia wewe Anaona kana kwamba umevaa nguo nyeupe za kupendeza (Ufunuo 19: 8).

Badala ya kuwaokoa ili wasirushwe ndani ya tanuru, Mungu aliwaokoa ndani ya tanuru. Kwa njia hiyo hiyo, wakati mwingine Mungu ataruhusu hali ngumu naakuokoe ukiwa ndani. Jinsi moto ulivyochoma kamba bila kuwadhuru, labda Mungu atatumia hali dhahiri ili kubadilisha moyo wako na kukupa uhuru wa ndani. Mungu anataka uwe na uhuru (Wagalatia 5:1).

Je, unakumbuka hazina ya uhusiano wa karibu na Mungu katika hali ngumu? Hapa tunaishuhudia tena, kwa sababu Mungu alikuwa pamoja nao motoni. Vivyo hivyo, Yesu tayari amekwisha kulipia gharama ya mwisho, na Yeye atasalia nawe katika hali yako.



YEAH!!

Ni kujiepusha na watu ambao walikutishia. Lakini Shadraka, Meshaki na Abednego walipotoka motoni, watu walijaa karibu nao na walishuhudia muujiza huo na wakamsifu Mungu. Hata hwakuwa na harufu ya moshi! Vivyo hivyo, ruhusu wale ambao walikutishia wakaribie ili waweze "kunusa" uwepo wa Mungu na uhuru kwako.

Ikiwa wangeogopa vitisho, hadithi hii ya ajabu haingekuwapo. Ilibidi wawe tayari kulipa gharama, hata ingawa hawakuwa na uhakika wa kile Mungu angetenda. Walibaki kama wanatazamia mbinguni na kuzingatia kuwa cha maana ni maoni ya Mungu.

Nachagua kulipa gharama ya kumfuata Mungu.




## SULUHISHO LA 9

Taffy alijibu kwamba bado hangeweza kushiriki, na kwamba angekubali alama za chini kutokana na hilo.

## SHUGHULI YA 9

**Utando wa buibui**




Shughuli hii ya kupendeza inasababisha hadithi ya kuchekesha. Anza na wanafunzi wote kama wameketi kama mduara, na umpe mwanafunzi mmoja mpira wa kamba. Mwanafunzi anaanza hadithi kwa sentensi 2 au 3. Kisha mwanafunzi anashikilia mwisho wa kamba na kutupa mpira kwa mwanafunzi mwingine. Mwanafunzi anayefuata anaongeza hadithi kidogo, anashikilia sehemu yake ya kamba, na kutupa mpira kwa mwanafunzi mwingine. Endelea hadi kila mwanafunzi awe na zamu na waunde utando. Halafu tendua utando na kuanza kuunda mpira tena huku wanafunzi wakiendelea kuongeza hadithi zaidi hadi utando uishe.


## MSTARI WA 9 WA WAKATI

Shadraka, Meshaki na Abednego walitupwa ndani na kuokolewa kutoka katika tanuru ya moto katika mwaka gani? Jibu: Katika mwaka wa 594 K.K. takriban.

## MAJIBU YA 9 YA MAFUMBO

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | U | F | I | N | I | M | A | A | W | F | M |
| A | G | B | D | O | G | I | K | K | L | U | O |
| R | F | U | H | G | U | K | E | T | A | H | S |
| W | A | N | O | E | M | A | M | U | N | U | H |
| A | R | M | F | N | L | H | O | G | N | R | I |
| M | E | A | U | D | Y | S | H | T | Y | U | S |
| I | A | M | D | E | M | E | C | G | Z | N | A |
| L | V | C | L | B | K | M | U | R | I | U | Z |
| E | S | A | B | A | S | O | K | P | M | T | I |
| I | O | C | M | N | F | U | A | L | E | O | J |
| N | N | B | U | A | L | M | O | M | O | S | U |
| A | A | N | I | K | A | R | D | A | H | S | U |
| D | A | I | R | C | A | K | A | L | M | A | M |





## MASWALI NA MAJIBU 9

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, uko tayari kulipa gharama gani kwa ajili ya ufalme wa Mungu?
Wacha wajadili jambo hilo. Mfano: Kubadilisha somo shuleni, kumuacha mpenzi wa kike au kiume, kwenda katika kanisa ndogo, kuhamia mji mwingine ili kuishi na mjomba na kuweza kuhudhuria shule nyingine, kuachana na marafiki, nk.
2. Je ni lazima nipende kila mtu?
Zungumzia kuhusu watu wanaofanya iwe vigumu kuwapenda, na ikiwa tunapaswa kulipia gharama ya aina hii.
3. Mungu anataka nini kutoka kwangu?
Zungumzia kuhusu malengo tofauti ya Mungu juu ya maisha yetu. Wengine wanaweza kusaidia ulimwengu kupitia taaluma zao kama wahasibu, madaktari, walimu nk. Wengine wanaweza kuingia katika huduma ya wakati wote, kama vile wachungaji, wamishonari, au wasimamizi wa huduma isiyo ya faida, nk. Zungumzia kuhusu tofauti kati ya kutoa kazi yako kwa ajili ya Mungu dhidi ya kutoa moyo wako kwa Mungu, jambo ambalo linasababisha kutoa kazi yako na kila sehemu ya maisha yako kwa ajili ya Mungu.

## MCHEZO WA 9



**Hakuna kucheka!**

Gawanya darasa katika jozi. Mtoto mmoja katika kila jozi atajaribu kumfanya mtoto huyo mwingine acheke. Sheria tu ni kwamba hawafai kumgusa mtoto huyo mwingine. Wape sekunde 30 kwa zamu hio, na mtoto yeyote ambaye hatacheka anashinda zamu hio. Acha watoto wabadilishe majukumu na kucheza tena.

## MAHUDHURIO YA 9




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Soma neno**

## KAZI YA 9 YA NYUMBANI

Chora picha ya mbinguni wiki hii. Waza kuhusu vitu vyote vinavyokupendeza sana hapa duniani: familia, vichezeo, mavazi, wanyama kipenzi, magari mazuri, anga, maua, nk. Mungu anaahidi kuunda mbingu mpya na dunia mpya (Isaya 65:17). Mungu yule yule mbunifu ambaye aliumba dunia hii ya kufurahisha na ya ajabu anaelekea kuumba dunia nyingine bora zaidi! Vitu vyote vizuri vitakuwapo na hakutakuwa na kitu kibaya. Weka picha yako kwenye ukuta katika chumba chako ili uweze kuikumbuka na kuiwaza, haswa unapokumbana na nyakati za kusikitisha.

**Soma**

Siku ya 1: Danieli 4:1-8
Siku ya 2: Danieli 4:9-18
Siku ya 3: Danieli 4:19-27
Siku ya 4: Danieli 4:28-33
Siku ya 5: Danieli 4:34-37

# 10. NYENYEKEA



**Hadithi ya Biblia:** Nebukadneza

Danieli 4

## FUNGU LA 10 LA KUMBUKUMBU

1 Wakorintho 4:7 Maana ni nani anayekupambanua na mwingine? Nawe una nini usichokipokea? Lakini iwapo ulipokea, wajisifia nini kana kwamba hukupokea?



## HADITHI YA 10 YA UHITAJI

Comet alikuwa amekaa wiki chache akionesha na kujisifu kwa sababu ya nywele zake na jinsi anavyoweza kukimbia haraka. Jambo hili liliwapa wasiwasi wanafunzi wenzake, na mwalimu akamwita na kumwonya kuwa tabia yako sio nzuri na kwamba lazima awe mnyenyekevu. Comet hakutaka kutii onyo hili.

## SOMO KUU LA 10

Leo katika Mashujaa wa Imani, tutaangazia mfalme maarufu na jinsi Mungu alivyomnyenyekeza. Mfalme Nebukadneza wa Babeli alikuwa na ndoto mbaya na akamwuliza mtu wa Mungu anayeitwa Danieli amtafsirie. Tutajifunza mengi kuhusu Daniel wakati ujao. Tafsiri hiyo ilikuwa kwamba mfalme angepata kichaa na kupoteza maarifa yake na kuishi nje kama mnyama anayekula nyasi. Mwaka mmoja baadaye, Mfalme Nebukadneza akaanza majivuno jinsi alivyokuwa amejenga mji mkubwa wa Babeli kwa ajili ya ukuu wake mwenyewe. Mungu anapokutumia kufanya vitu vyenye vinavyopendeza maishani mwako, itakuwa rahisi kila wakati kutazama mambo na kushangaza na mambo hayo na kusahau kwamba yalitoka kwa Mungu. Ukweli ni kwamba hakuna mmoja wetu aliye bora kuliko mwingine, kwa sababu kila kitu tulicho nacho - zawadi, talanta, uwezo, mafunzo, na fursa katika maisha yetu - zote zinatoka kwa Mungu (1 Wakorintho 4:7). Yesu alisema pia kuwa hatuwezi kufanya chochote kizuri bila Yeye (Yohana 15: 5). Mungu ndiye alifanya Nebukadneza kuwa mfalme, na kwa urahisi angeweza kuweka mtu mwingine kama mfalme. Mungu anaamua mambo ambayo atafanya kupitia maisha yako, na ana uwezo wa kutumia mtu mwingine kufanya mambo hayo. Wakati mfalme Nebukadneza alijivuna, alipoteza maarifa yake jinsi alivyoona katika ndoto yake na aliishi nje kama wanyama na kula majani. Alikuwa nje vya kutosha kiasi kwamba nywele za kichwa chake zilionekana kama manyoya na makucha yake yakawa marefu kama makucha ya ndege. Fikiria jinsi kucha zako zinavyochukua muda kuwa kubwa. Lazima mfalme huyo aliishi nje muda mrefu! Ndipo mfalme Nebukadneza alitazama mbinguni na akatambua kuwa mamlaka yote yanatoka kwa Mungu, na Mungu akamrejesha katika ufalme wake na akamfanya awe na nguvu zaidi. Lakini hupaswi kuchukua muda mrefu hivyo ili kuwa mnyenyekevu. Sisi sote ni wenye dhambi, na kiburi ni mojawapo ya dhambi rahisi kutenda, haswa wakati Mungu anafanya mambo yanayopendeza kupitia maisha yako! Hata ukipata majaribu kila siku, jitahidi na utazamie mbinguni na utambue kuwa kila kitu kizuri ulichonacho ni zawadi kutoka kwa Mungu (Yakobo 1:17). Unaweza kumwomba Mungu akupe usaidizi, kwa sababu anakupenda na anataka uwe bora zaidi. Mungu anaweza kukusaidia ili uwe mnyenyekevu.

Danieli pia alipendekeza jambo kwa mfalme ambalo linaweza kutusaidia ili tuwe wanyenyekevu. Danieli alimwambia aonyeshe neema kwa walionyanyaswa. Ni vigumu kujivuna wakati unashughulikia maslahi ya wanyonge. Unaweza kuwatazama ndugu na dada zako katika Kristo na utambue mambo mazuri ambayo Mungu anafanya kupitia maisha yao, pia, usijilinganishe nao bali watie moyo na ushereheke pamoja nao. Mungu hutupa vipaji vyote tofauti (1 Wakorintho 12:4-6), na Mungu atafanya mambo ya kupendeza kupitia sisi sote, hata hivyo anataka kuyanya Yeye mwenyewe.

Ninachagua kuwa mnyenyekevu na kutambua nguvu na mamlaka ya Mungu katika maisha yangu.


## SULUHISHO LA 10



Siku moja, kabla ya kufika shuleni ilianza kunyesha sana, na Comet alifanya awezavyo ili asilowe maji, na hakuweza kukimbia haraka sana ili azuie nywele zake zisiharibike.Alipoingia chumbani, kila mtu alimchekelea kutokana na jinsi alivyonyeshewa. Jambo hili lilimfanya ahisi vibaya sana. Kisha akaomba msamaha kwa wenzake na mwalimu wake na kamwe hakujisifu tena kuhusu nywele zake au kukimbia kwake.

## SHUGHULI YA 10

**Kuigiza kulingana na picha**




Gawanya darasa katika timu na utoe picha kwa kila timu. Timu inaangalia picha hiyo, ikijaribu kudhani kilichotokea kabla na baada ya picha kupigwa. Wape dakika chache za kuandaa. Kisha, kila timu inawasilisha mbele ya kikundi, ikiigiza kulingana na picha. Kundi litakalokuwa na wasilisho linavutia zaidi linashinda.

## MSTARI WA 10 WA WAKATI

Je, mfalme Nebukadneza alipata kichaa mwaka gani? Jibu: Katika mwaka 570 K.K. takriban.

## MAJIBU YA 10 YA MAFUMBO

| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | O | A | Z | E | N | D | A | K | U | B | E | N | E | M | L | A | F | M |
| M | U | N | G | U | B | A | H | D | A | S | O | M | O | L | A | M | U | N |
| A | N | M | G | O | A | M | S | B | S | S | M | A | Z | A | D | U | M | I |
| N | I | U | D | T | Z | A | I | U | M | I | R | A | K | U | S | G | L | R |
| U | R | A | Z | O | I | L | N | A | G | N | M | I | S | A | Y | N | A | U |
| V | I | S | I | D | O | T | U | F | I | S | I | J | U | K | L | U | I | B |
| I | S | D | A | N | I | E | L | I | O | I | T | O | N | O | A | M | T | I |
| J | A | T | I | O | G | A | S | P | A | C | H | O | G | O | L | I | A | K |
| U | F | I | L | A | G | N | M | U | V | E | K | E | Y | N | E | Y | N | M |
| K | U | K | A | N | D | A | M | I | Z | W | A | T | A | F | E | L | I | Z |







## MASWALI NA MAJIBU 10

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, mbona sio sawa kusema kwamba mafanikio yetu yanatokana na juhudi zetu?
Kwa sababu hio itakuwa kiburi, na Mungu anapinga wale walio na majivuno.
2. Je unyenyekevu unanisaidia vipi?
Kwa sababu tunapokuwa wanyenyekevu, Mungu atatusaidia. Tunapodahni kuwa sisi ni wakamilifu na kwamba mafanikio yetu yanatokana na juhudi zetu, Mungu atatupinga!
3. Kama haikuwa bidii yangu kufanikiwa au kupata kile nilicho nacho, nani aliniwezesha?
Mungu anataka tutambue kwamba usaidizi wetu unatoka Kwake. Vipaji na uwezo wote unatoka kwa Mungu. Wazazi wetu walitulisha, walitusaidia kwenda shule, nk. Watu wengine pia walichangia katika maisha yetu. Mungu hutufungulia milango, anatulinda dhidi ya mabaya, na lazima tutambue kuwa mafanikio yetu yanatokana na Mungu.

## MCHEZO WA 10



**Kutoroka!**

Timu za watoto 5. Kati ya hao, watoto 4 watashikana mikono kwenye mduara, na kumfungia mtoto wa 5 katikati. Mtoto aliye katikati ana dakika 1 ya kujaribu kutoka kwenye mduara wake. Baada ya kila zamu, watoto katika vikundi vyao wanabadilishana na mtoto tofauti anajaribu kutoka kwenye duara. Watoto ambao anatoroka kutoka mduara wake mara nyingi zaidi anashinda.

## MAHUDHURIO YA 10




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Mti Ulioanguka**

## KAZI YA 10 YA NYUMBANI

Fikiria kuhusu fursa na mambo mazuri ambayo umepata katika maisha yako. Mshukuru Mungu kwa ajili ya mambo hayo. Kisha fikiria kuhusu mtu ambaye atachukua mahali pako, kama vile mwanafunzi mdogo ambaye atachukua nafasi yako darasani mwaka ujao, na uwaombee ili Mungu awabariki katika nafasi hiyo na wafanye vitu vizuri katika maisha yao.

**Soma**

Siku ya 1: Danieli 6:1-5
Siku ya 2: Danieli 6:6-9
Siku ya 3: Danieli 6:10-14
Siku ya 4: Danieli 6:15-20
Siku ya 5: Danieli 6:21-28

# 11. IMANI KWANZA



**Hadithi ya Bibilia:** Danieli
Danieli 1, 6, 9:20-23

## FUNGU LA 11 LA KUMBUKUMBU

1 Petro 2:12 Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa.

## HADITHI YA 11 YA UHITAJI



Siku moja babake Peppy alifika nyumbani akiwa na huzuni sana.Aliwaeleza kwamba meneja wake aliona Bibilia kwenye dawati lake na akamwadhibu kwa hilo. Alimwambia kwamba vitu kama hivyo havifai kuwa kazini kwamba hataki kuiona ofisini tena wala kumsikia akiongea na mtu yeyote ofisini kuhusu Biblia. Alimtishia kwamba atapoteza kazi, ingawa huwa anafika kwa wakati na kila wakati alifanya kazi kwa bidii.Peppy na familia yake yote walianza kuomba kuhusu hali hii kwa sababu walihisi sio haki, na walitaka kumweka Mungu kama sehemu muhimu zaidi maishani mwao.

## SOMO KUU LA 11

Leo katika Mashujaa wa Imani, tutaangazia mtu ambaye alithaminiwa sana na Mungu. Lo, pongezi isio ya kawaida! Wacha tuangalie jinsi Danieli alivyofanya kazi kwa bidii katika kila jambo na akamudu kuzingatia imani yake kwanza.

Danieli alikuwa kijana wakati Wababeli walishinda Yerusalemu. Walimchukua yeye na marafiki zake ambao tuliangazia mapema hadi Babeli ili kusoma utamaduni wa Babeli kisha wafanye kazi kwa mfalme katika utawala na serikali. Wakati wa mafunzo, Danieli na marafiki zake walibadilishwa majina yao na kachukuliwa. Lakini hawakuruhusiwa wabadilishe chakula chao. Biblia haielezi sababu ya hatuo hio. Labda chakula hicho kilitolewa sadaka kwa sanamu, au kiliandaliwa kwa njia iliyo kinyume na sheria zao, au kilijumuisha nyama ambazo sheria yao ilitaja kuwa chafu. Licha ya hayo, Daniel alichagua kuweka imani yake kwanza. Kwa wakati, alipata afya njema licha ya vizuizi vyake vya chakula, na Mungu alimpa yeye na marafiki zake hekima na uelewa zaidi ya mtu mwingine yeyote. Danieli alitafsiri ndoto na alifanya kazi kwa bidii kwa kila mfalme katika falme za Babeli, Umedia na za Uajemi.

Miaka mingi baadaye, Danieli alimtumikia mfalme mpya Dario. Alifanya kazi yake vizuri sana kiasi kwamba Darius alipanga kumweka kama msimamizi wa mikoa yote ya ufalme wote. Wakuu wengine wakamwonea wivu na kujaribu kutafuta njia ya kumzuia. Lakini hawakuweza kupata kasoro yoyote katika mwenendo wake! Tunaambiwa tufanye vivyo hivyo, tuishi vizuri kiasi kwamba watu wanaotuzunguka watamsifu Mungu kupitia maisha yetu (1 Petro 2:12). Njia pekee y kumzuia ilikuwa kwa kutumia imani yake, kwa sababu kila wakati Danieli aliweka imani yake kwanza. Walitoa amri ya kukataza maombi kwa Mungu, na Danieli aliipuuza kabisa. Mfalme alijaribu kumwokoa, lakini kwa sababu sheria ilikuwa dhabiti sana, mfalme alilazimishwa kumfanya Danieli atupwe ndani ya tundu la simba. Lakini tena, Mungu alikuwa pamoja na Danieli ndani ya tundu la simba na malaika akafunga midomo ya simba, kwa hivyo hawakumla. Asubuhi iliyofuata, mfalme Dariyo alimpata Danieli akiwa

salama na hai na akamtoa ndani ya shimo. Maadui wa Daniel walitupwa ndani ya shimo na wakaliwa mara moja. Kisha Darius akasifu Mungu.

Yesu anatuomba tuzingatie imani yetu kwanza, au tuseme tumweke Yeye kwanza katika mambo yote. Lakini mara nyingi, kama Mafarisayo wa siku za Yesu, tunaweza kudhani kwamba ikiwa tunafanya mambo mazuri kanisani, ni sawa kuwatendea vibaya wengine. Jambo lilikasirisha sana Yesu (Mathayo 23:23). Mungu anapenda watu wote, na anajali jinsi tunavyowatendea. Hauwezi kutarajia wema wa Mungu wakati haujasamehe wengine (Mathayo 6:15). Na huwezi kumsifu Mungu na ulaani watu anaowapenda (Yakobo 3:9-12). Mungu anajali mambo unayochofanya ndani na nje ya kanisa, na tunaweza kumtumikia kwa kuwatenda wema kwa wengine na kufanya kazi nzuri katika kila kitu tunachofanya (Wakolosai 3:17). Halafu, ikiwa wakati unafika ambapo utahitajika kuchagua kati ya Mungu au wengine, chagua Mungu kwanza.

Nachagua kuweka Mungu kwanza, kwa kutambua kuwa Anajali jinsi ninavyowatendea wengine, pia.

## SULUHISHO LA 11



Siku moja msimamizi (mkubwa wa meneja) akaingia ofisini na akaona bibilia kwenye dawati la babake Peppy.Alisema anafurahia kusoma Biblia na alimpongeza babake Peppy kwa hilo.Kila mtu katika ofisi alisikia kuhusu hilo, na babake Peppy hakuwahi kuwa na tatizo lolote kutokana na kuwa na biblia.Hata wenzake hawakuogopa tena na walikuja na kuanza kuzungumza naye na kumuuliza maswali kuhusu imani yake. Familia ya Peppy iligundua kuwa Mungu alikuwa amebadilisha hali hiyo na alikuwa amejibu maombi yao na kuwasaidia kwa kuweka imani yao kwa Mungu kwanza.

## SHUGHULI YA 11

**Kuku kipofu**



Kwa shughuli hii, wagawanye wavulana na wasichana ili wacheze kivyao. Chagua mtoto mmoja kutoka kwa kila kikundi ili avae kitambaa cha kufunika macho. Watoto wengine wanaunda mduara na mtoto aliyefungwa macho anakuwa katikati. Weka mipaka ya kucheza darasani mwako. Mtoto aliyefungwa macho anawatafuta watoto wengine na anapaswa kukisia majina yao kwa kuwagusa tu.

## MSTARI WA 11 WA WAKATI


Je, Danieli alitupwa ndani na kuokolewa kutoka kwenye tundu la simba mwaka gani? Jibu: Katika mwaka 540 K.K. takriban.

## MAJIBU YA 11 YA MAFUMBO

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | U | N | G | U | A | G | U | N | F | G | A |
| A | F | G | U | I | N | O | L | I | B | A | B |
| G | A | A | U | O | M | I | H | S | I | M | F |
| I | K | U | L | B | E | H | B | K | A | I | F |
| S | H | D | I | M | A | N | I | A | I | L | I |
| H | I | U | N | O | E | M | M | M | I | E | T |
| E | M | B | Z | M | U | D | O | I | T | I | A |
| K | O | A | I | T | U | J | A | N | A | N | B |
| I | M | U | U | N | G | U | L | R | I | A | M |
| M | L | K | U | J | I | T | A | H | I | D | I |
| A | D | H | A | B | U | A | M | I | S | O | S |

| # | “ | % | $ | & |
|---|---|---|---|---|
| 35 | 20 | 30 | 27 | 40 |

| = | ? | ¡ | - | : |
|---|---|---|---|---|
| 30 | 23 | 27 | 23 | 25 |



## MASWALI NA MAJIBU YA 11

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, unaamini kabisa kuwa Mungu yupo, mbinguni ipo, kuzimu kupo, na kwamba siku moja kila mmoja wetu atakwenda aidha mbinguni au kuzimu milele?

Zungumza na wanafunzi wako kuhusu uzima wa milele na yatakuwa ya muda upi? Waulize ikiwa wanaamini kweli katika hilo, kwa sababu ni muhimu sana katika somo hili. Hatuwezi kuweka imani yetu kwanza maishani ikiwa hatuamini Mungu, mbinguni na kuzimu. Ikiwa tunaamini kwa kweli, basi ni rahisi kutambua kwa nini vitu vya uzima wa milele ni muhimu zaidi kuliko vitu vya ulimwengu huu.

2. Je, mbona kuna majaribu ya imani kama yale tundu la simba ambayo lazima tuchague imani kati ya hatari kubwa?

Kwa sababu ni rahisi KUZUNGUMZA kuhusu imani, lakini imani yetu itakuwa dhabiti zaidi ikiwa tutashinda majaribu magumu ambapo inatuhitaji tupuuze jambo muhimu kwetu.




YEAH!!

3. Je, unadhani Mungu hutujaribu na hali ngumu kwa kusudi? Kwa nini?
NDIYO!!! Ni kwa sababu Mungu anajua vizuri kwamba uzima wa umilele ni muhimu zaidi, na Mungu anataka tuimarishe imani yetu na kuwa Wakristo wakomavu.


## MCHEZO WA 11

**Sio kwa kuona**



Weka vifaa vyovyote kadhaa vya nyumbani katika mfuko wa kahawia. Fanya watoto waketi katika mduara kwenye sakafu. Watoto wanapaswa kufungwa macho kwa kitambaa na wachukue zamu ili kuondoa vifaa nje ya mfuko na kukisia majina ya vifaa hivyo. Wanaweza kujua kuwa tufaha ni tufaha, hata hivyo, hawawezi kuithibitisha bila kuiona. Wana imani tu kwamba wanajua wanachosema. Vivyo hivyo, watajua kuwa ni mpira wa pamba wakati wanaugusa kwa sababu wana uzoefu wa kutumia mipira ya pamba hapo zamani na wana imani kuwa wanachosema ni ukweli. Elezea watoto kwamba imani yetu kwa Mungu ni kama imani katika kuelewa vifaa vilivyo katika mfuko. Ingawa hatuwezi kuona Mungu kwa wazi, uzoefu wetu pamoja na Mungu hutusaidia kuwa na imani na kutambua kazi yake katika maisha yetu.

## MAHUDHURIO YA 11




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Danieli**

## KAZI YA 11 YA NYUMBANI

Omba peke yako kila siku wiki hii, hata ikiwa ni kwa dakika chache tu. Mshukuru Mungu kwa mambo mazuri katika siku hiyo na umwombe Mungu akusaidie kufanya vizuri shuleni na nyumbani. Fikiria kuhusu upendo wa Mungu juu ya maisha yako na umwambie unampenda, pia.

**Soma**

Siku ya 1: Yona 1:1-9
Siku ya 2: Yona 1:10-17
Siku ya 3: Yona 2:1-10
Siku ya 4: Yona 3:1-10
Siku ya 5: Yona 4:1-10

# 12. USITOROKE



**Hadithi ya Biblia**: **Yona**

Yona 1-4

## FUNGU LA 12 LA KUMBUKUMBU

Zaburi 51:10 Ee Mungu, uniumbie moyo safi,
Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu

## HADITHI YA 12 YA UHITAJI

Baba ya Kip alikuwa amemwomba asafishe chumba chenye uchafu zaidi ndani ya nyumba kwa ajili ya mkutano mchana huo. Kip alikasirishwa na agizo la babake, kwa sababu chumba hicho kilikuwa kichafu sana. Kisha alichukua kibao chake cha kutelezea na akaenda kutafuta marafiki zake.



## SOMO KUU LA 12

Katika Mashujaa wa Imani, tumeona kila aina ya njia za kumtumainia na kumtii Mungu. Je, nini hufanyika wakati Mungu anakuomba ufanye kitu ambacho hutaki kamwe kukifanya?

Mungu alimwagiza mtu mmoja anayeitwa Yona aende kuhubiri katika mji wa adui ulioitwa Ninawi. Yona alifunga mfuko wake na kwa furaha akaanza safari ya kwenda kuwaambia habari njema za neema ya Mungu - hapana!! Yona aliwachukia Waninawi na alitaka Mungu awaangamize. Badala yake, alijaribu kumkimbia Mungu. Tunapomwasi Mungu, huwa tunajaribu kutoroka au kujificha kutoka kwa Mungu kwa kukataa kuomba au kusoma Bibilia. Tunaacha kuwa waaminifu, kwa sababu tunahofia watu wajue ukweli kutuhusu, basi watatuona kama watu bandia. Inaweza pia kuonekana kama tunakasirishwa na kila kitu. Lakini ukweli ni kwamba tunapuuza na kumuasi Mungu. Yona akapanda meli kwenda Tarshishi, mbali na Ninawi jinsi angeweza. Dhoruba kubwa ilikuja hivi kwamba mabaharia wote na abiria wengine waliogopa sana. Wakati Yona alipoona kuwa hangeweza kumtoroka Mungu, aliwaambia wamrusha ndani ya bahari. Mungu alitoa samaki mkubwa aliyemeza Yona! Mungu anakupenda sana hivi kwamba atakutunza na hata atakusaidia ili uweze kumtii. Mungu alifanya samaki akamtapike ardhini, na alitii na akaenda Ninawi. Watu walisikia ujumbe wake na wakatubu, na Mungu hakuuharibu mji. Yona bado alikuwa anawachukia Waninawi na alikasirika kwa sababu Mungu aliwaokoa. Lakini Mungu anapenda watu wote na hataki yeyote apotee, ikiwa tu watatubu na watafute uso Wake (2 Petro 3: 9).

Je, utafanya nini ikiwa Mungu atakuomba ufanye kitu ambacho hutaki kufanya? Kama Yona, huwezi kumtoroka Mungu. Ikiwa haupendi watu ambao anakutuma kusaidia, jaribu mambo haya. Inaweza kubadilisha mtazamo wako unapowaombea (Mathayo 5:44). Unaweza kuzingatia vitendo walivyofanya dhidi yako au watu unaopenda, kisha uwasamehe na uache kuwa na matarajio yoyote kutoka kwao. Kumbuka kuwa Mungu hahitaji kulipwa ili akusamehe MAOVU ambayo umetenda. (Mathayo 18:21-35) Ikiwa hamasikizani na mtu fulani, waulize kuhusu mtazamo na ujaribu kuelewa. Na ikiwa watafanya jambo linalokupa wasiwasi, kagua moyo na matendo yako - utagundua hata wewe sio mkamilifu (Warumi 2: 1). Bila kujali sababu ya kukataa mwito wa Mungu, unaweza kumwomba Mungu akusaidie

ubadilishe moyo wako na umtii. Unapohisi kwamba hutaki kumtii Mungu, unapata fursa nzuri ya kubadilisha moyo wako.

Ninachagua kumtii Mungu hata wakati sitaki na kumwomba Mungu abadilishe moyo wangu.


## SULUHISHO LA 12



Alipokuwa akteleza katika bustani, moja ya magurudumu ya kibao cha kuteleza lilivunjika, na kusababisha Kip apate ajili na kuwaangukia baadhi ya marafiki zake. Mwanzoni Kip alikasirishwa na kibao chake, na marafiki zake kwa kusimama njiani, na yeye mwenyewe kwa kuteleza isivyofaa. Lakini alipoangalia kila mtu na kugundua jinsi kila mtu alivyoumia, Kip aliwaomba msamaha na kukubali kosa lake na kukiri kwamba hakufaa kuwa mahali hapo. Alirudi nyumbani, akaomba babake msamaha na akaanza kusafisha chumba.

## SHUGHULI YA 12

**Jina katika upande wako wa nyuma**



Tayarisha karatasi za rangi, wanyama, matunda, nk. na ugundishe karatasi moja kwenye mgongo wa kila mtoto kama "jina" lao na umpe kila mtoto karatasi na penseli. Kwa ishara yako, kila mmoja wa watoto anajaribu kunakili majina kutoka kwa migongo ya watoto wengine wakati akijaribu kuzuia wengine wasinakili jina katika mgongo wake. Hii itawafanya wazunguke, waruke na kila aina ya kusonga ili wazuie wengine wasinakili majina katika migongo yao. Baada kumalizika kwa muda, mtoto aliye na orodha ndefu zaidi ya majina anashinda.

## MSTARI WA 12 WA WAKATI

Je, hadithi ya Yona ilitokea katika mwaka gani? Jibu: Katika mwaka wa 790 K.K. takriban .

## MAJIBU YA 12 YA MAFUMBO

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| T | A | F | T | O | R | O | K | A | E |
| B | W | I | A | N | O | Y | D | T | P |
| K | E | C | R | S | N | A | H | U | U |
| E | L | H | S | A | U | I | O | B | K |
| B | O | A | H | M | H | W | R | U | A |
| M | K | T | I | A | T | A | U | T | I |
| U | O | J | S | K | T | N | B | I | L |
| J | U | U | H | I | E | I | A | A | E |
| U | K | T | I | M | G | N | V | M | M |

### KWELI AMA UONGO

Weka mduara kwenye herufi hii ikiwa jibu ni kweli na kwenye herufi ikiwa jibu ni la uwongo.

1. Samaki mkubwa akala Yona.
2. Wakati wote Yona aliwapenda watu wa Ninawi.
3. Mungu anakujali kila wakati.
4. Mwanzoni Yona alikuwa mtiifu.
5. Wakati mwingine Mungu hutuomba tufanye mambo ambayo hatutaki kufanya.



## MASWALI NA MAJIBU 12

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, itakuwa kumtoroka Mungu ikiwa hakuna mtu anayegundua?
Bila shaka. Au unadhani unaweza kujificha kutoka kwa Mungu? Kuwa na utani kidogo kwa kuzungumzia pamoja na wanafunzi wako kuhus sehemu tofauti ambazo tunaweza kujificha kutoka kwa wazazi au waalimu na uwezekano wa kujificha kutoka kwa Mungu. Kwa mfano, "Je, Mungu anaweza kukuona unapokuwa chini ya kitanda chako?"


2. Soma mfano katika Mathayo 13 na uamue ni ardhi gani ungependa kuwa nayo.
Fanya uamuzi. Je, ungependa maisha ambayo hutoa wema?
Baada ya kusoma mfano huo, chukua muda wa kuamua ikiwa unataka kuwa ardhi nzuri ambayo inaweza kuzaa matunda mara 100 zaidi ya mbegu zilizopandwa. Kwa kweli, tunaweza kurekebisha "ardhi" mioyoni mwetu ikiwa ina mawe au haina nafasi ya mizizi. Njia moja ya haraka ya kurekebisha ardhi yetu ni KUTII…. Na usitoroke wakati Mungu anakuomba ufanye jambo fulani. Kwa sababu katika visa vingi, Mungu anatuomba tufanye jambo kwa manufaa yetu, na tunapotoroka, tunamaliza matunda maishani.

## MCHEZO WA 12

**Lebo ya nyangumi**



Katika mchezo huu, mtoto ataiga nyangumi kwa kufungua na kufunga mikono yake kutoka juu hadi chini, na kuzunguka chumbani akijaribu kugusa watoto wengine.Kila mtoto ambaye ataguswa anaongezwa kama sehemu ya nyangumi na anaweka mkono wake kwenye bega la mtu aliye mbele yake na wanapanuka na kuunda mkia ambao unaweza kugusa watoto zaidi. Ikiwa mwishowe kuna watoto ambao bado hawajaguswa, wanapaswa kupigiwa makofi.




## MAHUDHURIO YA 12

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Yona**

## KAZI YA 12 YA NYUMBANI

Je, Mungu amekuwa akikuomba ufanye nini hivi majuzi? Je, kuna jambo ambalo unajua unapaswa kufanya lakini unaendelea kuahirisha au kulipuuza? Usisubiri na usilalamike. Nenda ulifanye.

**Soma**

Siku ya 1: Zekaria 7:1-7
Siku ya 2: Zekaria 7:8-14
Siku ya 3: Zekaria 8:1-8
Siku ya 4: Zekaria 8:9-13
Siku ya 5: Zekaria 8:14-23

# 13. TANGAZA UKWELI



**Hadithi ya Bibilia: Zekaria**

Zekaria 7-8

## FUNGU LA 13 LA KUMBUKUMBU

1 Wathesalonike 5:11 Basi, farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnavyofanya.

## HADITHI YA 13 YA UHITAJI



Hivi karibuni Buzz amekuwa akicheza pamoja na marafiki wapya. Marafiki hawa wamekuwa wakifanya jambo ambalo halimpendezi, mambo yanasababisha usumbufu kwa watu wengine. Kisha aliwaeleza kwamba aina hizo za michezo hazimpendezi, kwa sababu sio sawa kuwasumbua wengine. Walimcheka na kumwambia aende akacheze nyumbani.

## SOMO KUU LA 13

Wacha tuangazie shujaa mmoja wa mwisho wa Imani. Zekaria alikuwa nabii wakati ambapo Wayahudi walikuwa wakirudi kutoka uhamishoni kutoka Ufalme wa Uajemi. Zekaria, kama manabii wengine kwenye bibilia, alikuwa na jikumu la kutangaza ukweli, kutangaza Neno la Bwana kwa watu walio karibu naye. Wakati watu walikuja kumuuliza ikiwa wanapaswa kuendelea kufunga wakati wa kawaida, hakuogopa kuwaambia ukweli kwamba Mungu alizungumza naye. Hawakuwa wanafunga ili kumtafuta Mungu lakini kama ibada ili waonekane kuwa na imani. Vivyo hivyo, Mungu anaona mioyo yetu na anajua nia zetu kwa kila kitu. Na walikuwa wakiwatendea wengine mabaya huku wajifanya wenye imani kwa kufunga kula na kunywa. Mungu anachukia jambo hilo. Yesu aliwalaani Mafarisayo kwa kujifanya wenye imani wakati huo huo wakiwatendea wengine mabaya (Marko 12:40). Mungu alitumia Zekaria sio tu kwa kutambua mambo mabaya ambayo watu walikuwa wakifanya, lakini pia kuleta matumaini. Mungu alimtumia Zekaria ili ahamasishe watu wazingatie haki, rehema, na huruma kwa kila mmoja. Mungu anataka tuwasaidia wanyonge, tusiwaze mabaya kuhusu wengine katika mioyo yetu, tuseme ukweli na tutafute amani. Hawakuwa waache kufunga, lakini Mungu alikuwa anataka kubadilisha wakati huo uwe wa sherehe na furaha. Mungu alimtumia Zekaria mara kwa mara ili kutangaza ukweli, akiwakumbusha watu kuhusu mambo yote ambayo Mungu alisema hapo zamani, akiwahimiza wamtafute Mungu na watendeane vyema, na kutangaza kuja kwa Yesu.

Kwa njia hiyo hiyo, tunaweza kutiana moyo kupitia Neno la Mungu (1 Wathesalonike 5:11, Waebrania 3:13). Lakini huwezi kuwahimiza wengine na Neno la Mungu ikiwa haufahamu Neno la Mungu. Tumia wakati kusoma Biblia kila siku (Yohana 15: 5-8). Fikiria kama unaweza kukutana na mtu mgeni leo. Unawezaje kuunda urafiki mzuri Unahitaji kutumia wakati na mtu ili kuwafahamu vizuri. Kwa njia hiyo hiyo, unaweza kutumia wakati katika Neno la Mungu ili uweze kumfahamu Mungu mpaka awe rafiki yako bora zaidi - kisha uendelee kudumisha uhusiano huo! Ukristo sio kama shule ambapo unamaliza na kuhitimu kisha unamaliza. Kuna mengi zaidi yanayokusubiri na Mungu! Endelea kumfuata, kusoma Neno lake, kujifunza kutoka kwa Mashujaa wa Imani (kuna nyenzo zaidi ya zile tulizoangazia) na uhimize wengine kumfuata pia.

Ninachagua kuendelea kusoma Neno la Mungu na kuhamasisha wengine.

## SULUHISHO LA 13




Mama ya Buzz alipomuuliza sababu ya kuachana na marafiki zake, alimweleza kuhusu mambo waliokuwa wakifanya. Buzz aliamua kusalia nyumbani, na ingawa alikuwa peke yake, alihisi vyema, kwa sababu alikuwa ameongea ukweli.

## SHUGHULI YA 13

**Albamu ya kumbukumbu**

Sambaza kwa kila mtoto kipande cha karatasi kilichokunjwa. Katika upande mmoja, watoto wanapaswa kugundisha picha au kuchora picha. Katika upande mwingine, watoto wanapaswa kuandika jambo linalowahusu, kama vile fitina zao, micheo inayowapendeza, marafiki bora, nk. Mara tu baada ya kuunda Albamu zote, zichanganishe na uzisambaze kwa unasibu kati ya wanafunzi. Zisome kwa sauti kubwa na uonyeshe kila picha, na wanafunzi wote wanapaswa kukisia mmiliki wa albamu.




## MSTARI WA 13 WA WAKATI

Je, Zekaria alianza kutabiri mwaka gani ?Jibu: Katika mwaka 520 K.K. takriban .

## MAJIBU YA 13 YA MAFUMBO

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | K | U | S | O | M | A | P | O | T | S | I | R | K | U |
| K | U | O | N | G | G | I | R | R | Z | O | M | N | G | K |
| M | U | L | I | N | M | R | P | A | S | A | T | E | L | W |
| S | E | K | U | R | I | A | B | I | B | L | G | U | A | E |
| T | Y | F | F | I | L | K | R | E | W | K | U | N | M | L |
| Y | U | P | I | L | D | E | T | A | W | O | N | G | A | I |
| K | A | B | A | M | A | Z | G | I | F | H | M | U | N | T |
| O | A | Z | H | I | M | I | H | L | A | I | G | N | I | M |
| N | I | Y | D | E | A | M | A | B | I | M | K | A | R | I |
| K | A | E | U | O | N | G | O | I | V | I | U | I | G | U |
| M | Y | S | U | E | I | J | M | B | A | Z | C | R | E | R |
| U | J | U | Z | I | K | U | F | U | N | O | G | A | U | J |
| U | K | U | S | O | M | I | A | T | I | E | S | U | S | H |






## MASWALI NA MAJIBU YA 13

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, unahitaji kweli kusema ukweli hata kama utaadhibiwa na mwalimu kutokana na hilo?
Bila shaka, jibu ni ndiyo, lakini jaribu kuzungumza kuhusu hali tofauti wakati mwalimu angewakosoa. Kwa mfano, ni bora zaidi wakati mwalimu anamkemea mtoto ambaye hakusoma , kwa sababu hii itamsaidia mwanafunzi.Ikiwa mwanafunzi atasema uongo, hatapata usaidizi na atasalia vivyo hivyo.
2. Je, ni vizuri kusema uwongo ikiwa itamfanya mtu huyo mwingine ahisi vizuri, hapana?
Zungumza kuhusu hali tofauti na aina tofauti za uwongo. Jadili jinsi sifa bandia na maagizo yasiyo sahihi yanaweza kumfanya mtu huyo mwingine ahisi, lakini baada ya muda inaweza kumdhuru mtu huyo.
3. Je, ni rahisi kusema ukweli kila wakati, sivyo?
HAPANA, katika hali nyingi ni rahisi kusema uwongo kuliko kusema ukweli. Zekaria asingependa kutoa unabii mbaya, lakini ilibidi amtii Mungu na kusema kile Mungu alimwomba aseme kwa watu wake.

## MCHEZO WA 13

Kwa mchezo huu, tayarisha karatasi zilizo na majina ya mashujaa kutoka mtaala huu, za kutosha kwa kila mtoto.Weka karatasi ya shujaa nyuma ya kila mtoto bila ya wao kuona inahusu nini. Watoto wanapaswa kuchunguza na kukisia shujaa, kwa kufuata sheria hizi:



- Hawawezi kumuuliza mwanafunzi mmoja zaidi ya swali 1.
- Wanaweza tu kuuliza maswali 3 kwa jumla.
- Maswali yanapaswa kujibiwa aidha kwa 'ndiyo' au 'hapana'.

Mtoto yeyote anayefaulu kukisia anaweza kuweka karatasi mbele yake.

## MAHUDHURIO YA 13




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

**Utumwa**

## KAZI YA 13 YA NYUMBANI

Wiki kadhaa zilizopita, kazi ya nyumbani ilikuwa kusoma Biblia kila siku. Hii ni fursa yako tena! Soma Bibilia kila siku wiki hii angalau kwa dakika chache. Usiwe na wasiwasi ukikosa siku fulani lakini endelea kujaribu kuisoma kila siku na ujaribu kutenda kulingana na maandishi hayo. Je, ungependelea kusoma katika wakati gani wa siku? Unaweza kuweka bibilia karibu na kitanda chako au karibu na vichezeo vyako ili uweze kuifikia kwa urahisi kila wakati. Ikiwa una Bibilia kwenye kifaa chako cha mkononi, basi gundisha kipande cha karatasi mahali fulani ili kiwe kikumbusho, kama vile mlangoni katika chumba chako. Usitoe ahadi, kwa sababu sisi wanadamu huwa tunasahau kuweka ahadi mara nyingi. Unachohitaji tu ni kusoma Bibilia kila siku kwa maisha yako yote.

**Soma**

Hakuna kazi ya nyumbani.

Teacher Book Unit 3
Heroes
12132

www.ChildrenAreImportant.com
info@childrenareimportant.com
We are located in Mexico.
00-52-592-924-9041